Nipashe
Alhamisi Machi 25, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580530
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Hillary** Clinton ampongeza Samia kwa kuweka rekodi

UKURASA 3



**Adaiwa** kumuua rafiki yake kisa deni Sh. 3,000

UKURASA 5




**Ibrahimovic: Haikuwa rahisi kurudi Sweden**

UKURASA 20

# Hivi ndivyo mwili wa JPM utakavyozikwa

• **Vilio** vyatawala Mwanza, wavuvi wasimamisha shughuli... *Ukurasa 2 & 4*








Msafara wa gari lililobeba mwili wa aliyekuwa Rais Hayati Dk. John Magufuli, kwenye kivuko cha MV Mwanza, Ziwa Victoria ukitokea Kigongo wilayani Misungwi kwenda Busisi wilayani Sengerema, kuelekea wilayani Chato, mkoani Geita jana. **Picha ndogo:** Wananchi wa Mwanza, wakipanga matawi ya miti barabarani kama ishara ya kumuaga Dk. Magufuli, huku boti ya Polisi na mitumbwi ya wavuvi wakiisindikiza MV Mwanza iliyobeba mwili wa JPM. **Picha zaidi Uk. 10.**
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA 2

## BAKITA yasisitiza neno sahihi ni Amiri Jeshi Mkuu

**MICHEZO** **WATOA NENO DIMBANI BILA JPM** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Hivi ndivyo JPM atakavyozikwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imetoa nafasi kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa kuuaga mwili wa Rais John Magufuli, ili siku ya kesho iwe kwa ajili ya misa na maziko tu.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Mwanza wakati wa shughuli ya kuuaga mwili wa Rais Magufuli iliyofanyika kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, ikiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla.

Alisema wameamua kupita wilaya za Sengerema, Geita na maeneo ya Katoro, Bwanga na mwishowe wilayani Chato ili wananchi wamuage na kesho (Ijumaa) iwe ni maziko yatakayotanguliwa na misa kanisani alikokuwa akisali Rais Magufuli.

Kabla mwili huo haujapitishwa kwenye maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mwanza, wananchi waliobahatika kuingia kwenye Uwanja wa Kirumba, waliuaga mwili wa Dk. Magufuli uliozungushwa ndani ya uwanja huo kwa gari maalum.

"Utaratibu huu tunadhani ni mzuri kwa sababu ya idadi kubwa ya Watanzania wanaojitokeza kutamani kumuaga kiongozi huyu. Tumeona makundi mbalimbali huko, watoto wadogo, wanafunzi, vijana, wanawake na wazee wakitamani kumuaga.

"Ili kutoa nafasi, tumesema Jiji la Mwanza liandae barabara muhimu ambazo mwili utapita tuweze kuwafikia angalau mwili ukipita, muweze kulipungia jeneza," alisema.

Alitangaza kuwa mwili huo ulitarajiwa kupitishwa Nyegezi, Kwimba, Kigogo, Busisi nyumbani kwa Mke wa Rais Magufuli, Mama Janeth ambako walisimama kwa dakika 10 ili viongozi wa mila na dini watoe sala zao kwa muda mfupi.

**SALAMU ZA RAIS**

Akitoa salamu za Rais Samia Suluhu Hassan, Majaliwa alisema amewaomba Watanzania waendelee kushirikiana, kushikamana na kupendana kama ilivyokuwa awali.

Alisema Rais Samia amemtuma awaeleze wananchi kuwa katika kipindi hiki cha huzuni, ameomba wawe watulivu.

"Leo (jana) hii nimekuja na salamu za Rais wetu mpendwa Mama Samia, anawapa salamu za pole wana Kanda ya Ziwa wote, Mheshimiwa Rais amewasihi katika kipindi hiki cha huzuni, anawaomba sana kwanza tuwe watulivu, tuendelee kufanya shughuli hizi tukiwa bado tuna huzuni, tukisubiri kumfikisha kwenye nyumba yake ya milele," alisema.

Majaliwa alisema Rais Samia amemweleza kuwa ana matumaini katika kipindi hiki cha siku zote 21 za maombolezo, Watanzania watakuwa watulivu na kumwombea Rais Magufuli.

Alisema Mwanza ni sehemu ya kihistoria kwa Rais Magufuli kwa sababu amefanya kazi na kujenga uhusiano na watu mbalimbali na katika utumishi wake, amefanya mambo makubwa ambayo yameweka alama kwenye mikoa yote ya Kanda ya Ziwa na taifa.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulah, akitoa heshima za mwisho kwenye jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Rais Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza jana. **PICHA: OWM**

# BAKITA yatoa ufafanuzi wa Amiri Jeshi

**Na Christina Mwakangale**

SIKU chache baada ya kuibuka utata wa matumizi ya maneno 'amiri' na 'amirat' kutokana na Tanzania kupata Rais mwanamke kwa mara ya kwanza, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limetoa ufafanuzi kuhusu maneno hayo.

Ibara ya 33(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inabainisha kwamba kutakuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano, ambaye atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu.

Hata hivyo, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuapishwa kushika nafasi hiyo kubwa zaidi ya uongozi nchini, kuliibuka utata katika matumizi ya neno 'amiri', hoja kuu ikiwa ni kwamba neno hilo linatumika kwa mwanaume na kwa mwanamke anapaswa kuitwa 'amirat'.

Baada ya kutafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, baraza hilo kupitia kwa Katibu Mtendaji wake, Consolata Mushi, lilibainisha kuwa neno 'amiri' limechukuliwa kutoka lugha ya Kiarabu na halina mgawanyo wa kijinsia.

"Haina tofauti kati ya mwanamume na mwanamke, wengi wamekuwa na maswali. Unapochukua neno katika lugha uliyoichukua maana yake haiwi mbali katika ile maana ya msingi ya lugha yako.

"Amiri Jeshi Mkuu maana yake unamzungumzia kiongozi mkuu, yaani ni kiongozi mkuu wa jeshi, ambaye anasimamia majeshi yote nchini. Ana mamlaka ya kusimamia majeshi hayo. Tulilichukua kwa lengo moja, si kuligawanya kijinsia.

"Haina tofauti kati ya mwanamume na mwanamke, wengi wamekuwa na hili swali. (Mwandishi) si wa kwanza kuuliza hili swali, kwamba aitwe amirat? Hapana!

"Tulipolichukua neno 'amiri', tulimchukua kwa maana mkuu wa majeshi ya ulinzi na usalama. Hatukuchukua kama Kiarabu, amiri ni kwa wote. Awe mwanamume au mwanamke," alisema Mushi.

Alisema neno hilo linabeba maana moja kwa lugha ya Kiswahili na jamii inapaswa kuzingatia uongozi uliopo na cheo chake na si kuangalia neno lilikotoholewa na jinsia.

Kumekuwa na maswali kwenye mitandao ya kijamii kuhusu namna ya Rais Samia atakavyoitwa kijeshi huku baadhi ya vyombo vya habari vikianza kutumia neno 'amirat' kwa kiongozi huyo.

# ...Dk. Slaa afunguka anavyomjua

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

BALOZI wa Tanzania Sweden, Dk. Willibrod Slaa, amemzungumzia Hayati Rais John Magufuli, akibainisha anavyoufahamu utendaji kazi wake tangu mwaka 1995 walipoingia pamoja bungeni kwa mara ya kwanza.

Katika mazungumzo na Nipashe kwenye Uwanja wa Kirumba jana, Dk. Slaa alisema alifanya kazi kwa ushirikiano na Dk. Magufuli bungeni bila ubaguzi wa kikabila, udini na hata alipotembelea Jimbo lake la Karatu mkoani Arusha, hakuwahi kuwabagua.

"Hayati Dk. Magufuli ni mtendaji, kama mtu hana nidhamu, huwezi kuendana naye, huna kasi ya kufanya kazi wala kujua malengo yake katika nafasi aliyokupangia, hutaendana naye na hilo nimelithibitisha wakati aliponiteua katika nafasi ya kuwa Balozi Sweden," alisema.

Dk. Slaa alisema ameona mifano mingi ya kutokuwa na ubaguzi wa aina yoyote, iwe katika siasa, akitolea mfano wa uamuzi wa Dk. Magufuli kuwateua viongozi wa upinzani kushika nafasi mbalimbali ndani ya serikali akiwamo Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Dk. Kitilya Mkumbo, na Anna Mghwira kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro akitokea ACT -Wazalendo.

Alisema kuwa yeye mwenyewe aliteuliwa kuwa balozi akiwa hana chama chochote cha siasa baada ya kujiuzulu katika nafasi yake ya Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na hadi sasa hana chama chochote cha siasa.

Dk. Slaa alisema Hayati Dk. Magufuli alikuwa haangalii sura ya mtu, urafiki na hakuwa kiongozi wa maneno, bali alitaka mtu mchapa kazi na walionekana wala rushwa, wabadhirifu wa fedha za serikali, aliwakemea bila kuogopa na kuwatumbua pasipo kujali urafiki.

Alibainisha kuwa Dk. Magufuli alikuwa amewawekea utaratibu mabalozi wake wa kuhakikisha wanatuma taarifa za utendaji kazi kila baada ya miezi mitatu na kusoma taarifa hizo zote ili kujiridhisha na kile alichokutuma kukifanya. Dk. Slaa pia alisema alimfahamu Rais Samia Hassan baada ya kuteuliwa kuwa balozi wa kuhamasisha na kutoa elimu ya ugonjwa wa fistula ambao unawatesa kinamama.

Alisema jambo hilo ndilo lilimwibua Rais Samia na kuonekana kwamba anaweza kuchapa kazi, hivyo kiatu alichokivaa cha urais kwa sasa kinamfaa.

Dk. Slaa aliwataka Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali wanazozitengeneza mabalozi vinginevyo wataendela kuzisikia kama historia.





# Wanafunzi wamwomba asimamie elimu bure

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa shule ya msingi na sekondari Little Treasure, mkoani Shinyanga, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kusimamia sekta ya elimu bure na kuboresha miundombinu ya shule.

Walitoa ombi hilo jana wakati walipofika kutia saini kitabu cha maombolezo cha kifo cha Hayati Rais Dk. John Magufuli, katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga.

Mmoja wa wanafunzi hao anayesoma darasa la sita, Comfort Pius, alisema watamkumbuka Hayati Magufuli katika mchango wake mkubwa wa elimu, hasa katika suala la utoaji elimu bure na uboreshaji wa miundombinu.



"Tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassani kuendeleza yale ambayo ameyaacha hayati Rais John Magufuli, kwa kutoa elimu bure pamoja na kuboresha miundombinu ya shule, ili tutimize ndoto zetu," alisema Pius.

Mwanafunzi Janety Anthony, anayesoma kidato cha tatu katika shule hiyo, alisema utoaji wa elimu bure umesaidia wanafunzi wengi ambao wazazi wao hawana uwezo kwenda shule na kutimiza malengo yao.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Paulo John, alisema watamkumbuka Hayati Magufuli kwa mchango wake mkubwa kwenye sekta ya elimu kutokana na udahili wanafunzi kuongezeka shuleni.

Kaimu Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Dedan Rutazika, aliwataka wanafunzi wote nchini wasome kwa bidii na kufikia ndoto zao, ili kumuenzi Hayati Magufuli katika kukuza sekta ya elimu nchini.

**Tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassani kuendeleza yale ambayo ameyaacha hayati Rais John Magufuli, kwa kutoa elimu bure pamoja na kuboresha miundombinu ya shule, ili tutimize ndoto zetu**

# Hillary Clinton amtumia pongezi Rais Samia

**Na Salome Kitomari**


MKE wa Rais wa zamani wa Marekani, Hillary Clinton, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kushika nafasi ya juu ya uongozi wa nchi.

Hillary, ambaye ni mke wa Bill Clinton, ambaye alikuwa Rais wa 42 wa Marekani mwaka 1993 hadi 2001, pia aligombea urais kupitia Chama cha Democrat mwaka 2018 na kupambana na Donald Trump wa Republican lakini alishindwa.

"Kila la heri kwa Samia Suluhu Hassan, Rais mpya wa Tanzania na mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya juu ya uongozi wa nchi."

Samia ambaye kabla ya kuwa Rais, alikuwa Makamu wa Rais na amechukua nafasi hiyo kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu, katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu kutokana na maradhi ya moyo. Alikula kiapo kushika madaraka Machi 19, mwaka huu.

Hilary ambaye kitaaluma ni mwanasheria, pia ni mwanadiplomasia na aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wakati wa utawala wa Rais Barack



Obama mwaka 2009 hadi 2013.

Sambamba na wadhifa huo alikuwa Seneta wa Jimbo la New York, Marekani kuanzia mwaka 2001 hadi 2009.

Aidha, alikuwa mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwania nafasi ya urais na chama chake na katika kura za awali ndani ya chama mwaka 2016 akishindana na aliyewahi kuwa Seneta wa Jimbo la Vermont tangu mwaka 2007, Bernie Sanders.



Viongozi mbalimbali wakiwa jukwaani kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana wakati wa kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli kabla ya kusafirishwa kwenda Chato mkoani Geita kwa maziko yatakayofanyika kesho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwili wawasili Chato saa 12 jioni

**Na Richard Makore,** CHATO

HATIMAYE mwili wa Hayati Rais Dk. John Magufuli, jana uliwasili nyumbani kwake wilayani Chato, mkoani Geita na kupokelewa na umati wa wananchi uliotanda barabarani huku vilio na simanzi vikitawala.

Mwili wa Hayati Magufuli uliwasili saa 12 jioni huku msafara wake ukisindikizwa na helikopta mbili za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Wananchi walijipanga barabarani kuanzia mchana hadi mwili huo ulipowasili Chato saa 12 jioni, wakiwa wamebeba matawi ya miti, kinamama wakitandika kanga barabarani na wengine wakiangua kilio kwa huzuni.

Gari lililobeba mwili na mengine yaliyokuwa kwenye msafara yalipofika Chato, wananchi walionekana kusogelea msafara na kufanya barabara kuwa finyu wakiwa na hamu kuona kwa karibu jeneza lililobeana mwili huo.

Baada ya msafara kufika nyumbani kwake helikopta zilibaki zikizunguka angani kwa muda kadhaa.

Kwa mujibu wa taarifa ya serikali, leo wananchi watapata fursa ya kumuaga jemedari wao Hayati Magufuli na kesho kutwa Machi 26, maziko yatafanyika kijijini kwake.

# JPM aisimamisha Mwanza



Umati wa wananchi wa Kirumba, Ghana, Kiloleli, Nyasaka, Buzuluga, Mabatini, Mwanza mjini, Igogo, Mkuyuni, Nyegezi, Mkolani, Buhongwa na Usagara wakiwa wamesimama barabarani kuupokea mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, ulipowasili jijini Mwanza kwa ajili ya kuagwa katika Uwanja wa CCM Kirumba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Neema Emmanuel,**

**MWANZA**

MAELFU ya wakazi wa Mwanza na mikoa jirani, jana walijitokeza kuuaga mwili wa Hayati Rais John Magufuli, ulipowasili majira ya 1:31 asubuhi katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza, ukitokea Zanzibar.

Baada ya mwili kuondolewa uwanja wa ndege, vilio vilisikika kutoka kwa wananchi waliojitokeza kuupokea wakiwa wamejipanga kando ya barabara ya Makongoro kutoka uwanja wa ndege kwenda Uwanja wa CCM Kirumba.

Katika mapokezi hayo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliongoza viongozi mbalimbali wa serikali wakiwamo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Seleman Abdallah; Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika wa Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa CCM, Christopher Gachuma.

Wengine waliokuwapo ni Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro; na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella akiambatana na wakuu wa mikoa ya Mara, Adam Malima, Zainabu Terack wa Shinyanga na Brigedia Jenerali Michael Gaguti wa Kagera na viongozi mbalimbali wa chama na serikali.

> **“Aliyoyafanya ni kumbukumbu ambayo haitafutika katika historia ya taifa kuwa kulikuwapo na Rais wa awamu ya tano ambaye kupitia yeye mambo hayo yakawezekana.**

Kutoka uwanja wa ndege, msafara huo ulipita maeneo ya Ilemela, Sabasaba, Iloganzala, Pasiansi, Nyamanoro, Seleman Nassoro ambako aliwahi kuishi akiwa Waziri wa Ujenzi. Baada ya kufika eneo hilo, msafara ulisimama kwa dakika moja ili kutoa fursa kwa majirani zake kutoa heshima za mwisho.

Hatimaye msafara uliendelea kupitia Kona ya Bwiru, Ghana kupitia barabara ya Furahisha hadi CCM Kirumba ambako mwili uliingizwa ndani ya uwanja saa 3:17 asubuhi.

Baada ya kuwasili uwanjani, ilifuatia sala iliyoongozwa na Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mwanza, Renatus Nkwande, kisha dua maalum iliyosomwa na Sheikh wa Mkoa wa Mwanza, Alhaji Sheikh Hassan Musa Kabeke kwa niaba ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Mwanza.

**KAULI YA MAJALIWA**

Akizungumza na maelfu ya waombolezaji kabla ya kuuga mwili kuanza, Waziri Mkuu Majaliwa alisema Dk. Magufuli alikuwa kiongozi mahiri aliyeliongoza taifa kwa weledi mkubwa na kwamba vilio vya uchungu vya wananchi vinaakisi mazuri aliyoyafanya.

Majaliwa alsiema Mwanza ni eneo la kihistoria ambalo Magufuli aliwahi kuishi na kufanya kazi wakati wa uhai wake na amejenga makazi yake, hivyo ameacha alama kubwa kwa Kanda ya Ziwa kutokana na kazi alizofanya kwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Pia alivishukuru vyombo vya habari kwa kuripoti tukio hilo kwa kipindi chote tangu kutangazwa kwa kifo chake kuwa vimefanya kazi nzuri na serikali inathamini na kutambua mchango wao kipindi chote cha maombolezo.

Alisema Rais Samia Suluhu ana matumaini na Watanzania kuwa watakuwa wamoja na watulivu, hivyo wamwombee kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

**KAMA DAR, DODOMA**

Baada ya kumalizika kwa sala na hotuba ya Waziri Mkuu, mwili ulizungushwa mara tano kwenye Uwanja wa CCM Kirumba ili kutoa fursa kwa waombolezaji kutoa heshima za mwisho.

Baadaye uliondolewa tayari kwa safari ya Geita kupitia Furahisha ukipita barabara ya Makongoro, Ghana, Kona ya Bwiru, Nyamanoro, Pasiansi, Kiloleli, Montesori, Maduka Tisa hadi Buzuruga wilayani Ilemela.

Msafara huo baada ya Buzuruga uliingia Barabara ya Nyerere kupitia Mabatini, Mlango Mmoja, Natta, Mzunguko wa Mnara wa Mwalimu Nyerere hadi kwenye makutano ya barabara za Nyerere, Makongoro na Kenyatta.

Baadaye uliingia Barabara ya Kenyatta eneo la kituo cha mafuta cha Puma, Picha ya Samaki, Pepsi, VOIL, Mkuyuni, Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Nyashishi, Usagara Misungwi hadi kivuko cha Kigongo na kupandishwa kwenye pantoni hadi Busisi kwenda Sengerema.

Katika eneo la Busisi ambako ni nyumbani kwa wakwe zake (kwa wazazi wa mjane Janeth Magufuli), mwili ulisimama kwa dakika 10 ili kutoa nafasi kwa waombolezaji kutoa heshima za mwisho.

**WANANCHI WANENA**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi walisema taifa limepoteza mpiganaji na mtetezi wa wanyonge ambaye alikuwa mzalendo na mpenda maendeleo. Walisema daima watamkumbuka kwa aliyoyafanya katika kipindi chote cha uhai, uongozi hadi umauti ulipomkuta.

Mmoja wa wakazi wa mtaa wa Furahisha, Nyamwiza Mkatesi, alisema kila akitazama miradi ya maji na barabara zilizojengwa hasa maeneo ya miinuko, roho yake inamuuma sana.

“Aliyoyafanya ni kumbukumbu ambayo haitafutika katika historia ya taifa kuwa kulikuwapo na Rais wa awamu ya tano ambaye kupitia yeye mambo hayo yakawezekana. Leo (jana) nimeamua kufunga biashara yangu kuja kumuaga. Nimeumia, nimeumia sana,” alisema.

Naye Francis Dickson alisema kifo hicho kimehuzunisha mioyo ya watu wengi ambayo inashindwa kupokea na kukabiliana na jambo hilo zito la kuondokewa na kipenzi chao ambaye alipambana kwa dhati kulitoa taifa kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Dickson alisema Watanzania walikuwa na imani kubwa na Hayati Rais Magufuli kwa kuwa alionyesha mwanga na kufufua usafiri wa majini kwa kukarabati meli ya MV. Victoria na MV. Butiama, ujenzi wa meli mpya ambao unaendelea na ujenzi wa daraja la JPM lililoko Busisi.

# Adaiwa kuua rafiki kisa deni la 3,000/-

**Na Hamida Kamchalla,**

HANDENI

MKAZI wa Mtaa wa Bondo katika Kata ya Kwamagome, wilayani Handeni mkoani Tanga, Christopher William, anadaiwa kuuawa kikatili na rafiki yake kwa kucharangwa mapanga kutokana na deni la Sh. 3,000.

Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Kamishna Msaidizi Blasius Chatanda, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Machi 22, mwaka huu, majira ya usiku huko Handeni.

Alimtaja mtuhumiwa anayedaiwa kutekeleza mauaji hayo kuwa ni Samwel Alisei.

"Mwili wa marehemu Christopher umeharibika vibaya kutokana na majeraha makubwa mwilini na kwa hali ilivyo, imebidi tushauri kwanza azikwe jana (juzi) Machi 23 kutokana na marehemu huyo kutokuwa na ndugu Handeni.

"Baada ya muuaji kutekeleza unyama huo, polisi walifanikiwa kumtia mbaroni mtuhumiwa wa mauaji hayo na hivi sasa tunaendelea na mahojiano naye kabla ya kumpeleka mahakamani," alisema.

Akizungumzia zaidi tukio hilo, mke wa marehemu, Balbina Sure, alidai kuwa Machi 22 majira ya saa nne usiku, wakati mumewe akiwa ndani amelala, alifika mtuhumiwa na kumtaka aende nje, lakini yeye (mke) alimjibu, Christopher amelala."

Baada ya majibu hayo, mtuhumiwa wa mauaji hayo hakutaka kuelewa na kuanza kupiga kelele, akisema amefuata pesa yake.

Mjane huyo alidai kuwa kutokana na kelele hizo, mumewe aliamka na kwenda nje, ndipo walipoanza kujibizana huku kila mmoja akiwa ameshika panga na wakaanza kutishiana, mwisho mtuhumiwa alimzidi nguvu mwenzake na kumkata maeneo mengi ya mwili wake.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mji wa Handeni, Dk. Hudi Shehdadi, alisema kuwa baada ya kuufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, waligundua alijeruhiwa kwa kitu chenye ncha kali sehemu nyingi za mwili wake.

"Mwili tulipouangalia, kweli umekatwa na mapanga na tumeuchukua kwa uchunguzi zaidi, na baada ya hapo kwa taarifa zetu za kitaalamu zaidi tukimaliza, tutazipeleka polisi, nao watatoa majibu ya uchunguzi, lakini kwa jinsi mwili ulivyo, tunawashauri wazike kwa haraka," alisema.

Kutokana na tukio hilo, Diwani wa Kwamagome (CCM), Mussa Mkombati, aliwasihi wakazi wa eneo hilo kuacha kujichukulia sheria mikononi kwa kuwa madhara yake ni makubwa, ambayo ni pamoja na kusababisha vifo.

# Wanaokiuka agizo la vibali waonywa

**Na Christina Haule,** RUANGWA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ameuagiza uongozi wa Halmashauri za Wilaya za Ruangwa na Nachingwea mkoani Lindi, kumuweka ndani saa 48 mtu yeyote atakayekiuka agizo la kuchukua vibali na kukata misitu ya mbao kupitia vijiji ili kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu (FORVAC) na kutorudisha nyuma maendeleo ya vijiji husika.

Waziri Ndumbaro alisema hayo jana wakati akikabidhi mashine ya kuchakata magogo, yenye thamani ya Sh. milioni 110 iliyotolewa na Serikali ya Tanzania na Finland chini ya mradi wa kukuza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu (FORVAC) kwa vijiji 18 vilivyopo kwenye Wilaya za Ruangwa na Nachingwea mkoani Lindi.

Dk. Ndumbaro alisema ni vyema wananchi wakatambua kuwa vibali vya uvunaji wa misitu vinatolewa na vijiji pekee na atakayetaka kununua mbao lazima akatiwe na wanavijiji waliopo kwenye vikundi vinavyotambulika ili kufanya makusanyo ya kodi za vijiji na halmashauri kuwa mepesi.

"Naomba halmashauri zote zihakikishe manunuzi ya mbao yanafanyika kwenye vijiji vinavyozingatia uvunaji endelevu wa misitu, kwa wale waliopata elimu ya uvunaji misitu endelevu na sio vingine, mtu akitaka mbao anunue kwenye vijiji husika ili kuongeza mapato kwenye vijiji yatakayosaidia kuboresha maendeleo ya vijiji," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema makusanyo mazuri ya kodi za mazao hayo ya misitu kupitia FORVAC yatasaidia kuanzisha na kuboresha miradi ya vijiji na mradi wa FORVAC na halmashauri kuona haja ya kuongeza mashine zingine katika wilaya zingine zenye mradi wa uvunaji misitu.

"Licha ya kuongeza vipato vya wanavijiji mara mbili ya mwanzo, pia mashine hii inapunguza upotevu wa mazao ya misitu na kutengeneza ajira kwa wananchi na itazalisha ajira 250," alisema.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya zenye miradi ya masuala ya uvunaji misitu kusimamia miradi hiyo na kuhakikisha inafanya kazi na kuleta tija kwa wanavijiji wa wilaya husika.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

SALAMU ZA PONGEZI



Kamati ya Taifa ya Uongozi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF wanatoa pongezi za dhati kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Hongera sana Mama*

Mkurugenzi Mtendaji

**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**

S.L.P 2719 Dodoma, Tanzania

Simu: **+255 26 296 3866** Nukushi: **+255 26 296 3871**

Tovuti: **www.tasaf.go.tz** Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Tusijikite kwenye majina umakamu wa rais, bali sifa*

**WAKATI** taifa likiendelea na maombolezo ya siku 21 ya msiba mzito wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, baadhi ya watu wameanzisha mjadala husussan kwenye mitandao ya kijamii kuhusu mtu atakayerithi nafasi ya makamu wa rais.

Nafasi hiyo iko wazi, baada ya Samia Suluhu Hassan, aliyekuwa anaishikilia kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa katiba ya nchi.

Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 inaweka wazi kwamba baada ya Makamu wa Rais kuapa kuwa rais baada ya rais kuondoka madarakani kwa njia ya kifo kama ilivyotokea kwa Hayati Dk. Magufuli, anatakiwa kuteua jina la makamu wa rais baada ya kushauriana na chama chake kisha kulipeleka bungeni kuthibitishwa na Bunge.

Mjadala wa nani atakuwa makamu wa rais ni sahihi kabisa kuwapo hivi sasa kutokana na umuhimu wa nafasi yake katika uongozi wa kitaifa.

Hata hivyo, haitoshi kwa kutajataja tu majina ya watu wa kushika nafasi hiyo bila kutaja sifa zinazotakiwa. Makamu wa rais ndiye mshauri na msaidizi mkuu wa rais. Pale rais anapokuwa na shughuli nyingi, nyingine humtuma makamu wake kuzifanya au kumwakilisha.

Tukio la kifo cha ghafla cha Dk. Magufuli limekuwa fundisho kwetu na litapaswa kuendelea hivyo kwa vizazi vijavyo. Tunasema hivyo kwa kuwa kama katiba yetu ingekuwa kimya kuhusiana na rais anapofariki dunia, basi hali hiyo ingeweza kuzua mkanganyiko.

Kuhusiana jambo hili, hatunabudi kumkumbuka Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere aliyependekeza kuanzishwa kwa utaratibu wa kuwapo mgombea mwenza (Runing-mate) mwanzoni mwa miaka ya tisini, ambao ulianza kutumika kwa mara ya kwanza katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995.

Umuhimu wa nafasi ya makamu wa rais mi mkubwa ndio maana umezua mjadala huo, huku baadhi ya wanasiasa wanatajwatajwa kuteuliwa. Hata hivyo, jambo la msingi katika mjadala huo linapaswa kuwa ni sifa za mtu sahihi.

Jambo la kwanza ni kuangalia majukumu ya msingi ya kitaifa yanayomkabili Rais Samia kisha sifa za mtu anayeweza kumsaidia kwa maslahi ya taifa na sio yake binafsi na makundi au mitandao ya marafiki zake. Mengi tumeshayaeleza ambayo ni aliyoshaanzisha Hayati Dk. Magufuli na mengine ameyaacha kabla ya kuyakamilisha. Kwa maana hiyo Rais Samia anasubiriwa ayaendeleze na kukamilisha mengine.

Kwa kutaja baadhi ya sifa za mtu sahihi ni uadilifu, utiifu, kuchukia rushwa, kushehimu haki za binadamu, demokrasia, na utawala bora, mchapa kazi, mzalendo wa kweli, mbunifu, mwenye rekodi nzuri katika utendaji, mkomavu, mtulivu, anayeheshimika sana katika jamii, asiye na ubaguzi wa dini, rangi, itikadi za kisiasa nakadhalika.

Pia tunahitaji makamu wa rais ambaye atamsaidia Rais Samia kutatua kero za wanyonge, kusimamia ukuaji wa uchumi, nidhamu ya utendaji na uwajibikaji serikalini, anayeweza kumsaidia kurejesha uhusiano mzuri na jumuiya ya kimataifa na asiye na matamanio ya kuunda mitandao kwa ajili ya kusaka uongozi wa juu wa nchi.

Tunaamini Rais Samia ambaye ndiye mwenye jukumu la kumteua atazizingatia sifa hizi, ili aweze kukidhi matarajio ya Watanzania baada ya kuondoka kwa Magufuli, ambaye ameacha alama katika uchapaji kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# *Tangulia JPM, daima utabaki milele vichwani mwetu*

**TAIFA** bado lipo katika maombolezo kutokana na kifo cha Hayati Dk. John Pombe Magufuli alivyozoeleka 'JPM'.

Baada ya kutangazwa kifo chake Machi 17, mwaka huu, nchi ilizizima na ilikuwa ukitazama mwonekano wa watu katika maeneo tofauti tangu siku hiyo walio wengi wana simanzi usoni.

Imetia fora, kutokana na tangu ratiba ya mazishi ilipoanza jijini Dar es Salaam, Dodoma, visiwani Zanzibar na Mwanza, idadi ya waliojitokeza kuuaga mwili wake, imependukia.

Ushiriki wa viongozi kutoka mataifa mbalimbali hususan barani Afrika, mabalozi na taasisi za kimataifa kunadhihirisha upendo uliopo kati ya nchi na mwananchi mmoja mmoja kwa kiongozi wao.

Watanzania kuanzia viongozi ngazi ya mtaa, kata, kijiji, tarafa, wameshiriki kumwomboleza kiongozi wao, iwe kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii au kushuhudia ana kwa ana, inaweza kuwa kumbukumbu kwa vizazi na vizazi.

Pengine, inatokana na tukio hili kuwa la kwanza kutokea nchini, Rais kufariki dunia akiwa madarakani na kusababisha simanzi kwa Watanzania.

Matarajio ahadi na namna ya uendeshaji serikali yake ikiwamo utekelezaji na usimamizi wa ana kwa ana wa shughuli zinazogusa jamii, ikawa kumbukumbu inayobeba tukio hili kuongeza majonzi kwa Watanzania.

Lakini, uongozi wake Hayati Magufuli, ni alama na umetoa funzo kwa kila mmoja maishani mwake.

Pale walipohojiwa baadhi ya wananchi ikiwamo wajasiriamali, wamachinga, watumishi kupitia vyombo vya habari, wanamweleza kuwa ni kati ya viongozi wakuu, wananchi, walitoa elimu ya namna ya kuishi kwa kufuata kanuni na kuwa na nidhamu ya kila kitu hasa pesa.

Binadamu yeyote anaweza kufanikiwa, iwapo anakuwa na vipaumbele vyake, licha ya kila mwanadamu kuwa na mahitaji lukuki, kwa kuwa na bajeti maalumu inayoendana na kipato chake.

Wanasema kuwa, mfumo wa kuishi kwa kufanya kazi zaidi, kupitia falsafa yake ya hapa kazi tu, kulitoa morali ya kila mmoja kujishughulisha.

Kwamba palipo na fursa pakitumika ipasavyo kila mmoja atapata riziki yake, badala ya kusubiri cha kupewa na mtu.

Dhana hiyo aliyoijenga, waliotafsiri kwa mtazamo chanya na kuitumia, ndio hao kwa kiwango kikubwa ambao wanaonekana kwenye msafara wa kusindikiza mwili wa Hayati Magufuli, kumsindikiza katika safari yake ya mwisho duniani.

Mtindo wake wa kupita katika miradi tofauti, kuruhusu wananchi kuelezea kero zao awapo kwenye ziara zake, huku akiwataka viongozi wa maeneo husika kutoa majibu papo hapo, kumewaachia kumbukumbu wengi.

Hii pia inawakumbusha watumishi wa umma kuutumikia umma, ili kutatua matatizo yaliyopo ndani ya jamii kupitia elimu waliyoipata darasani.

Katika jamii yapo masuala muhimu ya kutiliwa mkazo na ndiyo kero katika jamii ambayo umma unasubiri serikali kuwatatulia. Mathalani, suala la maji, elimu, afya, barabara ni kati ya mahitaji ya binadamu husussan nchi zinazoendelea yanayohitaji kutatuliwa.

Huduma hizo kwa kiongozi yeyote ambaye anapata fursa kuutumikia umma zikipatiwa ufumbuzi ataacha alama ya kumbukumbu.

Katika hilo, JPM hatua ya kutoa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi sekondari, kumeokoa kundi la mabinti wadogo ambao walishindwa kufikia hatua hii kutokana na uchumi duni wa wazazi wao huku baadhi ya mila na desturi zikiwakandamiza.

Yapo, mengi lakini suala la elimu bure, kuongeza bajeti ya afya kumeokoa maisha ya kinamama na watoto kutokana na huduma kuboreshwa.

***Buriani mpendwa wetu JPM.***

## TANGAZO

# BURIANI



**HAYATI DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI**
**1959 – 2021**

Mtandao wa Wanawake Katiba, Uchaguzi na Uongozi, wenye zaidi ya Mashirika 200 ya utetezi wa Wanawake, Wasichana na Watoto, unaoratibiwa na Women Fund Tanzania Trust, unaungana na watanzania wenzetu, kutoa pole nyingi kwako Mheshimiwa Raisi, Samia Suluhu Hassan, viongozi wa Serikali, familia na watanzania wote kwa kuondokewa na aliyekuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli Raisi wa Awamu ya Tano (5).

Pia katika kipindi hiki cha maombolezo, ambacho tunaelewa ni kigumu sana kwako, na kwa Taifa zima, tunakuahidi kutoa ushirikiano wetu mkubwa katika kuendelea kumuombea Kiongozi wetu.

Tukiwa tunatambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli katika kukuza maisha na ustawi wa Jamii wakiwemo wanawake, wasichana na watoto katika Taifa letu, tunakutakia wewe binafsi na Viongozi wenzako **KHERI, HEKIMA NA WEPESI** wa kuendeleza yale yote Hayati Magufuli aliyoanzisha na aliyoyafanya nchini, ambayo kwa namna mbalimbali yaligusa maisha ya wengi, lakini zaidi maisha ya wanawake, wasichana, watoto na hasa wale wa ngazi ya chini.

**APUMZIKE KWA AMANI.**

MTANDAO WA WANAWAKE, KATIBA, UCHAGUZI NA UONGOZI

@womenfund_tz @wft.tz

# SALAMU ZA PONGEZI



**MTANDAO WA WANAWAKE, KATIBA, UCHAGUZI, NA UONGOZI** Mtandao wa Wanawake Katiba, Uchaguzi na Uongozi, ambao ni Mtandao wenye ushiriki wa zaidi ya Mashirika 200 yasiyo ya kiserikali na yanayofanya kazi za utetezi wa masuala ya haki za wanawake, wasichana na watoto, yakiwemo masuala ya kukuza uongozi wa wanawake nchini.
Tunachukua fursa hii KUMPONGEZA KWA DHATI, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita (6) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tukiwa Watetezi wa haki za wanawake, wasichana, watoto na wenye nia kubwa ya kuona utekelezwaji wa misingi ya USAWA WA JINSIA kama sehemu muhimu ya maendeleo na uongozi, tumefarijika sana kupata Rais wa kwanza Mwanamke kuliongoza Taifa letu.
Katika hili, nchi yetu imeweka KE-STORIA ya kipekee, ambapo imeonesha kwa vitendo utekelezaji wa nia ya kukuza ushiriki wa wanawake na kujenga misingi ya usawa wa jinsia katika ngazi mbalimbali za maamuzi nchini, zikiwemo nafasi za juu kabisa za uongozi wa taifa letu.

Tunatambua uwezo wako mkubwa wa kuliongoza taifa na kuendeleza misingi inayothamini michango na ushiriki wa wananchi wote. Umekuwa mfano mzuri wa kuigwa katika shughuli zako za kuliongoza taifa katika nyadhifa mbalimbali na tunategemea kuwa Viongozi wetu, wapenda maendeleo wote, wakiwemoo wanawake kwa wanaume watakaunganika nasi katika kuthamini na kutoa ushirikiano unaohitajika kwa Rais wetu wa Awamu ya Sita.

TUNAKUTAKIA AFYA NJEMA, HEKIMA NA UONGOZI ULIOJENGEKA KATIKA MISINGI YA KUJENGA UMOJA, MSHIKAMANO NA HESHIMA KWA WANANCHI WOTE - BILA YA UBAGUZI WOWOTE, UKIWEMO UBAGUZI WA JINSIA.

MTANDAO WA WANAWAKE, KATIBA, UCHAGUZI NA UONGOZI

@womenfund_tz @wft.tz

# WOMEN FUND TANZANIA TRUST (WFT Trust)

## SALAMU ZA PONGEZI



Wadhamini wa Bodi ya Women Fund Tanzania, Watendaji, na Wadau Wetu Wote, tunatoa Pongezi za Dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhemishimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa mfano wa kimsingi na wa kuigwa kuwa Raisi wa Kwanza Mwanamke nchini. Tunatambua uwezo, umahiri, na mchango wake mkubwa katika uongozi kwenye ngazi mbalimbali nchini. Hivyo tuna Imani kubwa na uongozi wake kuleta maendeleo nchini, kwa wananchi wote wakiwemo wasichana, wanawake na wanaume.

**Tunamtakia Heri na Baraka katika uongozi huu mpya.**
**HONGERA SANA**

**Women Fund Tanzania Trust**
**P.O.Box 79235**
**Dar Es Salaam**
**Office Mobile: (+255) 753 912 130**
**Tovuti: www.wft.or.tz / Email: info@wftrust.or.tz**

WOMEN FUND TANZANIA TRUST
Empowering Local Women Heroes

@womenfund_tz @wft.tz

# Viongozi wa dini wamlilia JPM

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

BAADHI ya viongozi wa dini mkoani Ruvuma, wametoa ya moyoni kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli (pichani), aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti juzi na jana, viongozi hao wamesema kifo cha Rais Magufuli ni pigo kubwa kwa Tanzania na kwamba Mwenyezi Mungu pekee ndiye anaweza kuisimamia nchi.

Sheikh wa Mkoa wa Ruvuma, Shaaban Kitete, alisema kifo cha Dk. Magufuli ni mtihani mkubwa kwa Watanzania wakiwamo viongozi wa siasa, serikali na wananchi hasa wanyonge ambao katika kipindi chake cha miaka mitano na miezi mitano, alisimama kidete kuwapigania na kuwatetea pale walipohitaji msaada.

Alisema viongozi wa serikali waliokuwa karibu naye, bado walikuwa wakihitaji kupata maelekezo yake yaliyokuwa yamejaa hekima za Mungu kwa ajili ya kuwasaidia wananchi katika maeneo mbalimbali.



Kitete alisema wakati Watanzania wakiwa kwenye maombolezo, Mwenyezi Mungu aendelee kuwasimamia ili wawe na faraja ambayo baadaye itakuwa na mwelekeo mzuri wa kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo.

Sheikh Kitete ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya Mkoa wa Ruvuma, inayounganisha dini zote, alitoa pole kwa serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM), familia ya Hayati Dk. Magufuli na Watanzania wote kwa msiba mkubwa uliowapata ambao hautasahaulika katika historia ya nchi.

Aliwashauri viongozi wahakikishe wanayafuata maelekezo yote aliyokuwa akiendelea kuyatoa wakati wa uhai wake na kwa kwamba wanapaswa kufanya mambo mazuri aliyokuwa akiyafanya.

Kiongozi huyo aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, zahanati, vituo vya afya na hospitali zinazoendelea kujengwa, usambazaji wa umeme kuanzia vijijini hadi mijini na upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

Naye Askofu Mkuu wa Kanisa la Redeemed Assemblies of God, Simon Silwimba, alisema katika utumishi wake, Dk. John Magufuli alikuwa na upeo mkubwa kwa kuona umuhimu katika shughuli mbalimbali alizokuwa akizifanya kuwa ni lazima amtangulize Mungu.

Silwimba alisema katika kipindi chake chote cha miaka mitano na miezi mitano mpaka mauti inamkuta, Dk. Magufuli alikuwa akihimiza maombi mbele za Mungu kwa kutoa siku maalumu za maombi na alipanua wigo mkubwa kwa wananchi kwa lengo la kumwomba Mungu ili kuiepusha nchi na majanga ukiwamo ugonjwa wa corona.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Ruvuma, Amoni Mwenda, alisema Tanzania Katika historia imepata pigo kubwa kwa kuwa Dk. Magufuli tangu alipochukua uongozi wa nchi hadi kifo, alikuwa ni mzalendo wa kweli.

Pia alisema alikuwa mfuatiliaji wa mambo mbalimbali ambayo utekelezaji wake ulikuwa mgumu na kwamba alikuwa na mipango mizuri ya kuiendeleza nchi huku akiwa na hofu ya Mungu.

Mwenda alitoa wito kwa Rais Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake waendelee kufanya kazi kwa bidii kama alivyokuwa anafanya kazi Magufuli huku wakiendelea kumcha Mungu ambaye ndiye muweza wa yote.

## Maduka ya vyakula, vipodozi yasajiliwa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Kusini, limesajili maduka ya vipodozi, vyakula na migahawa 601 katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma tangu lilipoanza kutekeleza jukumu hilo Julai, 2019.

Mkaguzi wa TBS Kanda ya Kusini, Buliro Magesa, alisema juzi kuwa katika ukaguzi uliofanyika kati ya Machi 3 hadi 17, mwaka huu, Manispaa ya Lindi, Kilwa na Mtama mkoani Lindi, shirika limesajili maduka ya vipodozi, chakula na migahawa 41, hivyo kufanya idadi kufikia 601 kutoka 560.

Magesa alisema TBS katika ukaguzi huo pia iliondoa vipodozi vyenye viambatasumu vya hydroquinon, madinitembo na zebaki pamoja na vyakula vilivyokwisha muda wa matumizi vyenye thamani ya Sh. 1,350,000.

Mkaguzi huyo alisema mpaka sasa Kanda ya Kusini imekwishapokea maombi 1,089 na kati ya hao wenye vibali vya usajili ni 601 na wasiona vibali ni 488.

Wakati huo huo, Ofisa Uhusiano Mkuu wa TBS, Rhoida Andusamile, alisema shirika litaendelea kusajili na kuthibitisha ubora wa bidhaa mbalimbali ikiwa ni utekelezaji wa jukumu lake la msingi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009.


**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**COMMERCIAL DIVISION**

**AT DAR ES SALAAM**

**MISCELLANEOUS COMMERCIAL CAUSE NO. 37 OF 2020**

**WINDING UP PETITION**

(Pursuant to section 281 of the Companies Act, No. 12 of 2002)

**IN THE MATTER OF THE COMPANIES ACT, No. 12 of 2002**

**AND**

**IN THE MATTER OF COMPULSORY WINDING UP OF WIA GROUP LIMITED**

(Made Pursuant to Rule 99 (1) of the Company (Insolvency Rules) G.N. No. 43 of 2005)

**TAKE NOTICE** that **VODACOM TANZANIA PLC (the "Petitioner")** of 15th Floor, Vodacom Tower, Ursino Estate, Plot No. 23, Old Bagamoyo Road of P.O. Box 2369, Dar es Salaam, on 17 September 2020 presented to the High Court of Tanzania (Commercial Division) a winding up petition praying for Orders under the Companies Act, No. 12 of 2002 to wind up **WIA GROUP LIMITED,** (**"the Company"**), of 2nd Floor, Barclay's House, Ohio Street, P.O. Box 5117, Dar es Salaam and appointment of an official liquidator of the Company.

The petition is scheduled for hearing at **the High Court of Tanzania (Commercial Division) at Dar es Salaam** on 1 April 2021 at 09:00 am before Honourable Nangela, J.

The Petitioner is being represented by **IMMMA Advocates** of IMMMA House, Plot No. 357, United Nations Road, Upanga, P.O. Box 72484, Dar es Salaam.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** any person intending to appear at the hearing of the petition (whether to support or oppose the petition) must give notice in accordance with the provisions of the Companies Act, No. 12 of 2002 and the Companies (Insolvency) Rules, 2005.

-------------------------

**Gaspar Nyika**

**Advocate for the Petitioner**



**TANGAZO LA KAZI**

**DEREVA DARAJA LA II- NAFASI 1**

**LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)** ni asasi isiyokuwa ya kiserikali inayopigania utunzwaji na umuduji mzuri na bora wa mazingira nchini. Hivi sasa LEAT inatekeleza mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID). Mradi huu unatekelezwa katika wilaya za Sumbawanga DC na NKasi Mkoani Rukwa. Ili kufanikisha kutimizwa kwa malengo ya Mradi LEAT inataka kuajiri Dereva mmoja (1) ili kuendesha gari la mradi.

**SIFA ZA KUAJIRIWA:**

1. Dereva awe na elimu ya Kidato cha nne(1V) Cheti cha kidato cha nne kutoka Baraza la Mtihani Taifa (NACTE) au elimu ya Darasal la saba aliyejienndeleza na kupata elimu ya ufundi wa magari na udereva kutoka chuu kinachotambulika na kutumia ujuzi huo kwa zaid ya miaka 15.
2. Mwenye leseni daraja la "C" ya uendeshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitano bila kusababisha ajali.
3. Mwenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II na uwezo wa kufanya matengenezo ya kawaida ya gari;

**KAZI ZA KUFANYA:**

1. Kuendesha gari la mradi wakati wa utekelezaji wa kazi za mradi na shughuli za ofisini;
2. Kuhakikisha gari na vifaa vyote vipo katika hali nzuri wakati wote na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo madogomadogo katika gari.
3. Kutunza na kuandika daftari la safari "Log-book" kwa safari zote.

**SIFA ZA JUMLA**

1. Muombaji ni lazima awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 35 na usiozidi miaka 50.
2. Muombaji ni lazima aambatanishe cheti cha kuzaliwa, vyeti vya ujuzi, vyeti vya taaluma na wasifu wake.
3. Barua za maombi ya kazi yandikwe kwa mkono.
4. Awe tayari kufanya kazi mkoani;
5. Muaminifu,mwadilifu, mwenye nidhamu ya hali ya juu;
6. mkweli, na asiyetumia kilevi; na
7. Asiye na rekodi yoyote ya kosa la jinai.

Maombi haya yatumwe na kufika ofisi za LEAT zilizopo Mikocheni "B" Mtaa wa Mazingira kabla ya tarehe 08 Mwezi wa Aprili,2021 saa kumi na moja jioni.

Maombi yote yatumwe kwa kupitia barua-meme ifuatayo: **info@leat.or.tz**
Aina nyingine yoyote ya mawasiliano tofauti na iliyotolewa hapo juu haitapokelewa na haitachukuliwa kama maombi rasmi,

**Imetolewa:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Lawyers Environmental Action Team (LEAT)**
**Mazingira House, Mazingira Street**
**P. O Box 12605, Dar es Salaam**
**info@leat.or.tz**

TANGAZO

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)

### WARAKA MIZANIA ULIO HAKIKIWA KWA TAREHE 31.12.2020

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | MWAKA WA SASA 31.12.2020 | MWAKA ILIYOPITA 31.12.2019 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,545 | 2,955 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,184 | 21,842 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 20,280 | 21,172 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 34,926 | 32,749 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 132,804 | 113,652 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,649 | 3,378 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,264 | 1,349 |
| 16 | **Jumla ya Mali** | **211,652** | **197,097** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 24,256 | 5,847 |
| 18 | Amana za Wateja | 140,666 | 149,691 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 74 | 183 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 46 | 38 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | 36 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,385 | 1,898 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **168,427** | **157,693** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **43,225** | **39,404** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 28,607 | 27,277 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,697 | 1,103 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 921 | 1,024 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **43,225** | **39,404** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 9,423 | 12,413 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,943 | 2,495 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,689 | 893 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 20% | 20% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2% | 2% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 82% | 74% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 63% | 58% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89% | 85% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 6% | 17% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 7% | 14% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI ILIYOHAKIKIWA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2020 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2020 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 15,166 | 14,811 |
| 2 | Gharama za Riba | 5,317 | 4,843 |
| 3 | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **9,849** | **9,968** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | 896 | 4,036 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 34 | 464 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **1,445** | **1,906** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 430 | 618 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,002 | 1,278 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 13 | 10 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **5,112** | **5,639** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 2,269 | 2,427 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 540 | 625 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 2,303 | 2,587 |
| | 7.4 Other Provision | - | - |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **5,252** | **1,736** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 1,555 | 634 |
| 10 | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **3,697** | **1,103** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **3,697** | **1,103** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **48** | **49** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 370 | 110 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2% | 1% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 9% | 6% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 45% | 47% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6% | 7% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA ILIYOHAKIKIWA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2020

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI |
|---|---|---|---|
| | | **31.12.2020** | **31.12.2019** |
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 5,252 | 1,736 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | - | - |
| | -Hasara katika Mali | 1,128 | 685 |
| | -Prior Period Adjustment | 124 | (1,002) |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (20,047) | (15,543) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | (4) | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 9,384 | 17,533 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,350 | 5,637 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (2,113) | 3,915 |
| | -Kodi Iliyolipwa | (1,555) | (634) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | 275 | 110 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **(6,206)** | **12,438** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (1,174) | (42) |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | 892 | 2,196 |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(282)** | **2,154** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** |
| IV | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **(6,488)** | **14,591** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 45,898 | 31,307 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **39,410** | **45,898** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI ILIYOHAKIKIWA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2020

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **28,381** | **775** | **-** | **249** | **39,404** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 3,697 | - | - | - | 3,697 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (103) | 103 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | 124 | - | - | - | 124 |
| Revaluation Reserves | | | | | | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **32,099** | **878** | **-** | **249** | **43,225** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,103 | - | - | - | 1,103 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 3,209 | (3,209) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 937 | - | (937) | - | - |
| Mengineyo | - | - | (1,002) | - | - | - | (1,002) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **28,381** | **775** | **-** | **-** | **39,156** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2020**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir<br>(Mkurugenzi Mtendaji) | | 8th March, 2021 |
| Deogratias Edward Ndushi<br>Mkuu wa Fedha | | 8th March, 2021 |
| Mwita Mohamed Mwita<br>(Mkaguzi wa Ndani) | | 8th March, 2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni<br>(Mkurugenzi) | | 8th March, 2021 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava<br>(Mkurugenzi) | | 8th March, 2021 |

# MWANZA WAMUAGA HAYATI JPM



Mwili wa Hayati Dk. John Magufuli, ukiwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Mwanza, jana. **PICHA: OWM**



Gari maalum lililobeba mwili wa Hayati Dk. John Magufuli likiingia katika Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza jana, kwa ajili ya kuagwa. **PICHA: ROSE JACOB**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na wananchi wa Mwanza wakati wa tukio la kuaga mwili wa Hayati Dk. Magufuli. **PICHA: OWM**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa Dk. Magufuli. **PICHA: OWM**



Wananchi wakiwa wametandika kanga chini ili gari lililobeba mwili wa Dk. Magufuli lipite, baada ya kutoka kwenye kivuko cha MV Mwanza, eneo la Busisi wilayani Sengerema jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkurugenzi Mtendaji wa TBL Plc, Philip Redman, akitia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, katika ofisi ya mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




# Azifanya zahanati, vituo vya afya na watumishi wake kuzaliwa upya

## • Madaktari wakiri kuna 'mageuzi ya kweli'

**Na Peter Orwa**


Siku Rais Dk. John Magufuli, alipozindua Kituo cha Afya Madaba, mkoani Ruvuma. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI ameacha nafasi yake akiwa na miaka mitano na miczi kadhaa katika uongozi, kabla mapenzi ya Muumba kutimia, Hayati Dk. Magufuli tayari alishafanya makuu katika sekta ya afya.

Kuna usemi wa Kiswahili kwamba 'usione vyaelea, vimeumbwa.' Yapo mengi aliyofanya, pia ni mwendelezo wa ama mawazo au matendo ya Rais mtangulizi wake, Mzee Jakaya Kikwete.

Ni aina ya mfumo ambao umechukua nafasi katika uongozi wa kisiasa kitaifa, sasa ikiwa awamu ya tano, anapokomea mmoja, mwingine anaendeleza kwa kasi mpya anayoanza nayo.

Baada ya kurithi kwa ufanisi mkubwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), iliyopitia awamu mbili za utekelezaji, mzizi wake ukiwa utawala wa Hayati Benjamin Mkapa, Rais Kikwete, alibeba uzoefu wa MMEM, akaanzisha Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), uliopitishwa mwaka 2007 na kuanza rasmi 2008.

Rais Kikwete, msomi ya uchumi aliyedumu katika nafasi Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano Kimataifa kwa miaka 10, akaweka sehemu ya mitazamo ya utekelezaji wa MMAM katika sura kuu kadhaa.

Hapo ni kila kijiji au mtaa kuwa na zahanati, kata inakuwa na kituo cha afya, ila kwa kinachonufaika kuwa na kituo cha afya, hakipatiwi tena zahanati na ilipanda katika kila wilaya kuwa na hospitali, huku zile za mkoa kuwa za rufani.

Vivyo hivyo, kila kanda inakuwa na Hospitali ya Rufani ya Kanda na Muhimbili (MNH), na tawi lake la Mloganzila, Dar es Salaam, zinakuwa hospitali ya taifa.

### SAFARI YA JPM

Baada ya kuingia madarakani, Rais Dk.Magufuli alichukua hatua za ziada kufuatilia kwa karibu huduma za jamii, hata katika muundo wake mpya wa kiserikali, aliamua Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuwa chini ya ofisi yake.

Hapo moja kwa moja, huduma za ustawi wa jamii ikiwamo elimu na afya ikijumuisha MMAM, alihamishia ofisini kwake, kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Kupitia uamuzi huo, ni pale ananuia kuelekeza jicho katika utekelezaji wa ilani yake ya uchaguzi, pia mikakati binafsi katika usimamizi sahihi aliyonuia.

Itakumbukwa, hata Waziri Mkuu wake wa sasa, KassimMajaliwa, akawa kivutio chake, alitokea TAMISEMI katika awamu iliyopita ya serikali.

Pia, hadi umauti hakuficha kusifu ufanisi wa waziri wake wa TAMISEMl, Selemani Jafo, aliyeshikamana mwenye Wizara ya Afya, Ummy Mwalimu, hadi walionyesha cheche ya ufanisi.

Katika safu iliyopo, Rais Dk. Magufuli, alitoa ufafanuzi wa sifa kubwa ya mafanikio ya Waziri Ummy, katika awamu ya pili akimhitaji kwa kazi maalum, katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Nafasi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, alimpandisha Mtendaji Mwandamizi, Dk. Dorothy Gwajima, kuwa waziri na kumpatia ubunge.

Akizungumza katika hafla ya Siku ya Madaktari Tanzania Februari, mwaka jana, Dk. Magufuli alisema mfumo wa uwekezaji katika sekta ya afya, unalenga kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa dawa na vifaa tiba, kuifanya Tanzania kuwa kimbilio la wagonjwa kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Pia, alisema hiyo inafanyika kwa kuongeza idadi ya rasilimali watu, vifaa tiba pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu.

Katika mabadiliko hayo, mfumo wa ununuzi kutoka Bohari Kuu ya Serikali (MSD), ulijengewa unafuu wa bei elekezi kwa mtumiaji, kwa sababu dawa ziliagizwa moja kwa moja kutoka kwa wauzaji.

Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka minne ya utawala wake, serikali iliajiri watumishi wapya 13479 wa sekta ya afya.

Katika ufafanuzi wake, aliwaambia madaktari kwamba, hadi kufikia Julai 2019 walikuwapo watumishi wa kada ya afya 98,987 waajiriwa kati yao 18,904 wako katika sekta binafsi

Hiyo alisema, ilienda sambamba na kuimarisha na kuboresha miundombinu ya huduma za afya, kwa ujenzi na ukarabati wa zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya katika maeneo mbalimbali nchini.

### ZAHANATI/ VITUO AFYA

Rais Magufuli aliwaambia madaktari hao kwamba, kumeongezeka idadi ya zahanati kutoka 6044 mwaka 2015 hadi kufikia 6467 Januari 2020, ikiwa nyongeza ya 423; zahanati 4922 ni za serikali.

Vituo vya afya navyo vimeongezeka kutoka 718 mwaka 2015 hadi 1169 mwaka 2020, ikiwa ni nyongeza ya 451; Mgawanyo wa miliki zake, 887 vinamilikiwa na serikali na vituo 282 vya sekta binafsi. Pia, Rais Magufuli alisema serikali iliongeza idadi ya vituo vya afya vyenye uwezo wa kufanya upasuaji kutoka vituo 115 mwaka 2015 hadi kufikia vituo 467 Januari 2020.

"Serikali pia imekarabati hospitali za Halmashauri 22 katika miundombinu yote jumla ya Sh. bilioni 293.7 zilitumika, sambamba na kununua vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 68.706.

"Pia, kukarabati hospitali za rufaa za mikoa 23 kwa thamani ya Sh. bilioni 89.5 pamoja na kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Mloganzila," alitamka Rais Dk. Magufuli.

### RAIS WA MAT

Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Elisha Osati, alikiri kuwapo maboresho ya kiasi kikubwa katika huduma za matibabu kwa wananchi, akisema:

"Tulipokuwa tukisoma tuliona vifaa vingi katika mafunzo kwa vitendo, lakini kwa sasa katika kila kona ya nchi kuna mageuzi makubwa yanayoendelea kufanyika na tunaishukuru serikali kwa kuendelea kuwa karibu na MAT na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya afya nchini."

# MAPINDUZI MAKUBWA NDANI YA MUHIMBILI

**• Kila alichoagiza ziara ya ghafla 2015 zimetekelezwa • Miaka minne; dawa zapatikana 96% kutoka 40% • Upasuaji kihistoria, ubia rasmi na Mloganzila • Wazunguka kugawa ujuzi hospitali zote za mikoa**

**Na Peter Orwa**

MARA baada ya kuingia madarakani, Rais Dk. John Magufuli, alifanya ziara kadhaa za ghafla katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kukagua maendeleo ya utendaji.

Ni staili aliyotumia katika siku zake za kwanza za uongozi, kukagua mengi. Mojawapo aligundua moja ya wodi ya wazazi kutumiwa kama ofisi.Aliagiza wahame mara moja.

Mnamo Novemba, mwaka 2015, siku chache baada ya kuapishwa, alifanya ziara ya kushtukiza na hakuficha hali ya huduma kwa wagonjwa hususan wanaolala chini.

Pia, alikuta baadhi ya vifaa vya kufanyia kazi na mashine muhimu za uchunguzi wa magonjwa kama vile MRI na CT-SCAN vilikuwa havifanyi kazi kwa muda wa miezi kadhaa.

Baada ya hapo kuna hatua kadhaa zilichukuliwa na Rais ikiwamo, kuhamisha ofisi zilizokuwa ndani ya wodi ya wazazi na kupaboresha, ikiwamo kuwapo kwa vifaa vya kuhudumia wagonjwa kama vile vitanda.

Pia, ndani ya kipindi kifupi mwaka 2016, kulishuhiwa mageuzi makubwa ndani ya Hospitali za Muhimbili na Mloganzila kwa maboresho ya vifaa na huduma, alipofika kumjulia hali mkewe, pamoja na mke wa Balozi na Waziri Mstaafu, Omar Ramadhan Mapuri, waliolazwa katika wodi ya Sewa Haji, wagonjwa walimshukuru kwa maboresho ya serikali.

Walibainisha kuwa, licha ya kuboreshwa kwa mazingira ya hospitali, pia walikiri kupata huduma nzuri kutoka kwa madaktari na wauguzi.

### MAVUNO YA JPM

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Lawrence Museru, alipozungumzia miaka minne ya mafanikio yake, tangu uongozi wa Dk. Magufuli, anasema wamefanikiwa kutekeleza maagizo saba ya Rais John Pombe Magufuli.

Hapo anaorodhesha upatikanaji wa dawa kwa kiwango cha asilimia 96 wakati ilikuwa katika asilimia 40 pekee; kutoa huduma za ubobezi katika kupunguza rufaa nje ya nchi; wagonjwa waliokuwa wakilala chini kupatiwa vitanda; ulipaji stahiki za wafanyakazi.

Mengine anayataja kuwa ni kuboresha mazingira ya kazi; kununua na kukarabati vitendea kazi; na kuondoa kero ya vifaa vya uchunzi vya MRI na CT-scan.

Rais Dk. John Pombe Magufuli, alitekeleza muda mfupi tu baada ya kuingia madarakani mwaka 2015, alipofanya ziara ya ghafla, lengo kubwa ni kukagua uhalisia na kuboresha huduma za matibabu hospitalini Muhimbili.



Vitanda na mahitaji mengine yakihamishiwa wodini, baada ya ofisi kuondolewa kwa agizo la Rais Dk. John Magufuli. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **"ongezeko la vyumba hivyo, imesaidia kupungua msongamano katika upasuaji, hata kurahisisha utoaji huduma kwa watoto kutoka mara nne hadi mara 10 kwa wiki.**



Kazi ya kuhamisha vifaa vya kiofisi kutoka sehemu ya wodi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mkurugenzi Mtendaji Prof. Museru, anasema katika uwekezaji uliolenga kutekeleza maagizo ya Rais Dk. Magufuli, MNH ilitumia Sh. bilioni 37.4 kununua vifaa tiba na mashine, kuboresha miundombinu na kujenga uwezo wa wataalamu.

### HUDUMA UPANDIKIZAJI

Prof. Museru anasema kuwa, MNH iliokoa Sh. bilioni 32 kwa kutoa huduma ya upandikizaji figo kwa wagonjwa 51 tangu walipoanzishwa kwake, Novemba 2017.

Mkurugenzi huyo, pia anataja huduma ya upandikizaji vifaa vya kusaidia kusikia kwa wagonjwa 34; huduma ya magonjwa ya mfumo wa chakula na ini, zimeshatolewa kwa wagonjwa 380; na upimaji wa radiolojia kwa wagonjwa 558 tangu wakati huo, Novemba 2017.

Mkurugenzi Mtendaji amefafanua kwamba katika kipindi cha miaka minne, hospitali imetumia Sh. bilioni 72 kununua dawa na kusaidia wagonjwa kupata dawa kwa asilimia 96 tofauti na awali dawa zilikuwa zikipatikana kwa asilimia 40.

Pia, anasema wagonjwa walikuwa walikutwa na Dk. Magufuli wakilala chini, hivi sasa wamepatiwa vitanda na tatizo hilo limekwisha, hata mojawapo wagonjwa wa Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), kuhama kutoka wodi za MNH.

Awali wagonjwa hao walikuwa wanazitumia wodi mbili ndani ya jengo la Sewa Haji na mojawapo katika jengo la Mwaisela, sasa ni chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum 'ICU' yenye vitanda 15.

### HUDUMA YA UPASUAJI

Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), mwaka 2018 ilifanya upasuaji mkubwa wa watoto pacha walioungana sehemu ya tumboni na kufanikiwa kuwatenganisha watoto wachanga wenye jinsia ya kiume.

Ni upasuaji uliotumia saa tano, ulifanywa na wataalamu wenyeji wa upasuaji Muhimbili na wadau wao, kwa kushirikiana na wenzao kutoka Ireland.

Prof. Lawrence Museru, anasema hospitali imefanikiwa kufanya upasuaji kwa mafanikio na kwamba uliwezekana baada ya kuboreshwa miundombinu ya huduma katika vyumba vya upasuaji, pia elimu kwa wataalamu husika.

Anasema, ongezeko la vyumba hivyo, imesaidia kupungua msongamano katika upasuaji, hata kurahisisha utoaji huduma kwa watoto kutoka mara nne hadi mara 10 kwa wiki.

Kwa mujibu wa Prof. Museru, baada ya watoto hao kufikishwa Muhimbili, walilazwa katika chumba cha ICU, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kufanyiwa upasuaji wa kuwatenganisha.

Daktari Bingwa wa Upasuaji Watoto, Petronila Ngiloi, anasema walishirikiana na wataalamu wa upasuaji kutoka Ireland, katika kuhakikisha watoto hao wanatenganishwa, lengo likiwa kupunguza hatari yoyote wakati wa upasuaji.

Pia, Bingwa wa Upasuaji wa Watoto, Dk. Zaituni Bokhary, anasema ni mafanikio yaliyohusisha timu ya wataalamu 10 wa upasuaji watoto, wauguzi na wataalamu wa tiba ya usingizi.

"Nashauri watoto pacha walioungana au wenye matatizo ya kiafya waletwe Muhimbili ili wafanyiwe uchunguzi wa kina na baada ya kujiridhisha tutawapatia huduma stahiki," anaesema Dk. Bokhary.

### UPASUAJI MIKOANI

Madaktari Bingwa wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kushirikiana na wataalam wa afya wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mtwara- Ligula, mwaka 2018 walizuru huko na kuwafanyia upasuaji wagonjwa 10 wenye matatizo ya mafindofindo (shida kooni).

Matibabu hayo ya kibingwa hayafanyiki katika Hospitali ya Ligula, kutokana na ukosefu wa wataalamu waliobobea katika maeneo ya pua, koo na masikio.

Daktari bingwa wa upasuaji pua, koo na masiko kutoka Muhimbili, Willybroad Massawe, anasema waliwafanyia upasuaji watu wazima na watoto.

"Tumeanza kufanya upasuaji huu leo asubuhi na lengo letu ni kumaliza wagonjwa wote kumi leo hii" alisema Dk. Massawe.

Mtaalamu huyo alisema, mafindofindo yanasababishwa na maambukizi ya kila mara katika njia ya hewa na kwa wengine inatokana na mzio (allergies) uliokithiri.

### HUDUMA ZA MIKOBA

Daktari Massawe, alisema alipokuwa Ligula - Mtwara, kwamba Muhimbili ina programu ya kutoa huduma kwa njia ya mkoba, kwa nia ya kuzijengea uwezo hospitali za rufani za mikoa, katika maeneo yenye wataalamu wenye uhitaji huo ili kupunguza rufani za wagonjwa kwenda nje ya nchi.

Pia, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Mpoki Ulisubisya, alishaagiza wakati huo hospitali ya Muhimbili, kuendelea kutoa huduma za mkoba katika hospitali za rufani na baadaye iwe kitaifa.

Ni kauli aliyoitoa akiwa mkoani Mara kufungua huduma kwa njia ya mkoba, ilipotolewa na wataalamu wabobezi wa Muhimbili kwa kushirikiana na wenzao katika Hospitali ya Rufani ya Musoma.

Dk. Ulisubisya aliwahimiza watalaamu wabobezi wa Muhimbili kuzuru hospitali nyinginezo za rufani nchini, ili kuwajengea uwezo katika huduma mbalimbali za afya ambazo zimeshindikana.

Katika tafsiri pana, pia aliwataka wajuzi hao kwenda nje ya nchi kwa ajili kutoa huduma za afya na kubadilishana uzoefu, akiwa na maelekezo ya kuwataka kufika nchini Comoro.

Rai ya Kaibu Mkuu iliwafikia viongozi mbalimbali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wajisajili katika taasisi husika na kupatiwa vitambulisho vya bima ya afya.


Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Lawrance Museru.

> **"Hospitali ya Musoma, ilifanikiwa kufungua duka la dawa la hospitali, kuanzisha huduma za kibingwa kwa kutumia madaktari kutoka Hospitali ya Bugando na kununua kompyuta 40.**

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Joachim Eyembe, alisema wakati huu mwaka 2018, hospitali yake ilikua na watumishi 306, wakiwa na upungufu wa watumishi 375 sawa na upungufu wa zaidi ya mahitaji (asilimia 55.1).

Pia, alisema hospitali ya Musoma, ilifanikiwa kufungua duka la dawa la hospitali, kuanzisha huduma za kibingwa kwa kutumia madaktari kutoka Hospitali ya Bugando na kununua kompyuta 40.

Mkazi wa Mkoa wa Mara, Easter Juma, alisema wamekuwa na matatizo ya siku nyingi hivyo wameiomba serikali ipeleke wataalamu bingwa katika hospitali hiyo kila baada ya miezi minne.

Pia, Yusuph Abdallah Chamba, mkazi wa Musoma alieleza kufurahishwa na huduma hizo za kibingwa za mikoa walizofikishiwa na aliiomba serikali kuongeza wataalamu zaidi hospitali hapo.

### USTAWI WA WATUMISHI

Prof. Museru anasema, ndani ya kipindi hicho cha miaka mine ya mwanzo ya uongozi wa Rais Dk.Magufuli, Muhimbili ilitekeleza agizo lake kwa kuwalipa wafanyakazi malimbikizo ya madai yao waliokuwa wanadai kwa kipindi kirefu, ikiwamo wito wa kikazi, kazi za wauguzi usiku na posho mbalimbali, hasa kwa madaktari na kada nyinginezo za afya.

"Kutolipwa kwa wafanyakazi, hali hii ilishusha morali kwa kiwango kikubwa sana na hivyo wafanyakazi kupunguza kasi ya ufanyaji kazi, hivyo tija kukosekana. Kwa sasa wafanyakazi wengi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili wana ari ya kufanya kazi," anaeleza.

Pia, Prof. Museru anasema kwa nyakati tofauti hospitali hiyo kati ya mwaka jana na mwaka 2015, ilipeleka wataalamu mbalimbali nje ya nchi, kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

Anasema ni orodha inayojumuisha madaktari bingwa, wauguzi, wataalamu wa maabara, wataalamu wa radiolojia, magonjwa ya mfumo wa chakula na ini, watalaam wa saratani za damu, ili kupata ujuzi na elimu ya kutoa huduma hizo kwa ufanisi.

"Mafunzo haya yameigharimu Muhimbili Sh. bilioni 3.597, hivyo Watanzania wengi wamehudumiwa nchini, badala ya kupelekwa nje, pia imekoa kiasi kikubwa cha fedha za Serikali za umma," anasema Prof. Museru.

KUKABIDHIWA MLOGANZILA

Prof. Museru anasema tangu Oktoba 3, mwaka 2018, MNH ilikabidhiwa kusimamia hospitali ya Mloganzila na tayari imefanikiwa kufanya upasuaji mkubwa wa kuondoa uvimbe katika mishipa ya damu kwenye ubongo.

Hapo anasema, wakati gharama za upasuaji kwa mgonjwa mmoja nje ya nchi ni wastani wa Sh. milioni 40, nchini imegharimu Sh. milioni 20 na kwa wagonjwa wanne waliohudumiwa, wamegharimu Sh. milioni 80, badala ya Sh. milioni 160 za nje za nchi. Kwa maana hiyo, kumeokolewa Sh. milioni 80.

Mkuu huyo wa Hospitali Muhimbili- Mloganzila, anasema, wamekuwa hospitali ya pili ya umma nchini kufanya upasuaji wa matatizo ya mgongo (spinal surgery), baada ya MOI.

"Tangu kufunguliwa kwa Hospitali hii ya Mloganzila, wagonjwa 869 kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili wamepokewa hospitalini hapa (Mloganzila) na kupatiwa huduma, hatua ambayo imepunguza msongamano wa wagonjwa Muhimbili," anasema.

Kuhusu mipango ya baadaye, Prof. Museru, anasema hospitali yake inakusudia kujenga jengo la ghorofa tatu kwa ajili ya wagonjwa binafsi (IPPM), litakalokuwa na vyumba 20 vya kulala mgonjwa mmoja mmoja.

Pia, kutakuwapo vyumba 20 vya kulala wagonjwa wawili; vyumba vitano vya kulaza watu mashuhuri (VIP) na cha kulaza viongozi wa kitaifa, maarufu 'presidential suite.'

***Makala hii ni kwa mujibu taarifa mbalimbali, zikiwamo rasmi za Hospitali ya Taifa Muhimbili. Kesho usikose makala kuhusu Rais John Magufuli na mfumo wake wa kiuchumi.***




IBADA YA PAMOJA..

# Wakazi Handeni wakusanyika kumlilia, kumuenzi JPM, wamwombea Rais Samia

## • DC, viongozi wa dini, wazee wanena

**Na Mashaka Mgeta,** Handeni

WAKATI taifa, Afrika na sehemu za dunia zikiendelea kuomboleza kifo cha aliyekuwa Rais John Magufuli, wakazi wa Handeni mkoani Tanga, wameungana kwa ibada ya pamoja.

Ni tukio lililojumuisha waumini wa madhehebu yote, kumwombea dua kiongozi huyo aliyedumu madarakani kwa takribani miaka mitano na miezi nne.

Ibada hiyo ilifanyika juzi kwenye uwanja wa Shule ya Msingi Chanika wilayani humo, ikahudhuriwa na viongozi wa dini, serikali, vyama vya siasa; wakiwa ni miongoni mwa wengine kwa maelfu, ilitumika pia kumuombea heri katika majukumu yake mapya, Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa ibada hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Toba Nguvila, aliainisha mambo 35 yanayoelezea mafanikio na maisha ya Magufuli, kisha kuomba umma wa Tanzania kuendelea kumuunga mkono Rais Samia.

Nguvila aliyataja mambo hayo katika makundi ya kuchochea uwepo wa nidhamu serikalini, ubunifu na usimamizi wa miradi ya maendeleo ikiwamo ya kimkakati na namna 'dunia' inavyojua Magufuli, kiasi cha marais wengi kumuita 'shujaa wa Afrika'.

Kwa mujibu wa Nguvila, miongoni mwa uamuzi thabiti na usimamizi imara katika uongozi wa Magufuli ilikuwa katika kudhibiti safari za nje ya viongozi wa serikali, kukomesha mianya ya rushwa na kuwaadhibiti waliotumia vibaya madaraka yao kupitia mtindo maarufu wa 'kutumbua majipu'.

**VIONGOZI WA DINI**

Mchungaji Abel Ngoda wa Jumiya ya Kikristo Tanzania (CCT) anasema sifa zinazotolewa baada ya kifo cha Magufuli, ni matokeo ya mambo mazuri aliyoyafanya wakati wa uhai wake.

Hivyo, Ngoda anasema hali hiyo inatoa funzo kwa wanadamu kutenda mambo mema wakati wa uhai, ili wanaobaki wasitafute uongo wa kutunga ili kupata 'sifa za marehemu'.

Mchungaji Ngoda anasema, ni lazima wanadamu kuendelea na maisha ya kawaida baada ya kifo na ipo haja kwa Watanzania kuendeleza mshikamano na kuunga mkono mamlaka zilizopo, hususani Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi waliopo kwenye serikali yake.

Sheikh wa Wilaya ya Handeni, Shaban Kizulwa anasema taifa limeondokewa na mtu muhimu na akatoa wito kwa Watanzania kuzidi kuiombea heri serikali ya Rais Samia, katika kuendeleza kazi zilizoachwa na hayati Magufuli.

Anasema, wema kiimani kwa Mungu, umedhihirika kwa ishara nyingi, ikiwamo kufanikisha mchakato wa kukabidhi madaraka kwa Rais Samia, kwa amani, utulivu na umoja kitaifa.

> **Tumuombee Rais wetu huyu (Samia) Mwenyezi Mungu amzidishie ujasiri, ili aweze kuongoza na kuzipita njia za mtangulizi wake Baba yetu Magufuli tunayeendelea kuomboleza kifo chake.**



Sehemu ya umati uliokusanyika kumwombea. **PICHA ZOTE: MASHAKA MGETA**



Padri Daniel Mwambashi wa Kanisa Katoliki, Parokia ya Handeni, alipokuwa kwenye ibada ya kumwombea Hayati Rais John Magufuli.

"Tumuombee Rais wetu huyu (Samia) Mwenyezi Mungu amzidishie ujasiri, ili aweze kuongoza na kuzipita njia za mtangulizi wake Baba yetu Magufuli tunayeendelea kuomboleza kifo chake," akasema.

Sheikh Kizulwa anasema, utendaji kazi wa pamoja kwa viongozi wakuu kabla ya kifo cha Magufuli, ulikuwa salama, hivyo ni wajibu wa kusimama na kutoyumbishwa kwa hila zozote.

"Tumuombee sana Rais wetu Samia aendelee kumtegemea Mwenyezi Mungu, na kwa vile hatukupata kusikia dosari yoyote kati ya viongozi wetu wakuu wa nchi, na yeye pia (Samia), azidi kupata kuungwa mkono ili atimize vema majukumu yake," anasema.

Padri Daniel Mwambashi wa Kanisa la Katoliki, Parokia ya Handeni, anasema kuna mengi ya kujifunza katika uongozi wa maisha binafsi, ikiwamo hulka za ushupavu, ujasiri, uadilifu na ujemedari.

Padri Mwambashi anasema, kuondokewa na kiongozi aliyekuwa katika nafasi ya juu ya utawala wa nchi, ni vyema Watanzania wakafarijiana, kwa vile kila raia amejeruhika kwa kuondokewa na Magufuli.

Kiongozi huyo wa kiimani, anasema ipo haja kwa Watanzania kuendeleza vipaji vyake katika uongozi, kuchagiza kasi ya maendeleo na ustawi wa wananchi.

"Magufuli amefanya mambo mengi katika kipindi kifupi cha utawala wake akiwa Rais wa nchi...tusisononeke sana kwa maana ni mapenzi ya Mungu mwenyewe kumtwaa kutoka kwetu," anasema.

Mchungaji Ahia Godwin wa Kanisa la Adventista Wasabato, anasema mfumo na maisha ya Hayati Dk. Magufuli, ulitoa funzo katika nyanja tofauti za maisha, hivyo anapaswa kuendelea kuenziwa kwa vitendo.

"Baba huyu (Magufuli) alikuwa zaidi ya muelekezaji, zaidi ya kiongozi wa dini na kwa kifo chake, imekuwa mfano wa kipigo tulichokipata kutoka kwa ibilisi," anasema.

Kwa mujibu wa Mchungaji Godwin, kifo kinapaswa kuendelea kuwa ishara kwa watu kujiandalia maisha ya raha mbinguni, kupitia matendo mema na kuwajali wahitaji hususani watu wanyonge.

**WAZEE HANDENI**

Katika adhimisho la ibada hiyo, wazee mashuhuri wa wilayani Handeni, wakiwakilishwa na Bonaventura Mhina na Mama Lydia Mhando, walihimiza Watanzania kuendelea kumuombea Dk. Magufuli na baraka zaidi kwa Rais Samia, katika uongozi wake wa awamu ya sita.

Mhina, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wazee katika Mamlaka ya Handeni Mji, anamfafanua Dk. Magufuli, alikuwa mtetezi wa wazee, kazi aliyoifanya kwa kushirikiana na Rais Samia (alipokuwa Makamu wa Rais), hivyo hakuna shaka kada hiyo itaendelea kuangaliwa, kutetewa na kutimiziwa mahitaji yao.

"Tunatambua Magufuli alishirikiana kwa karibu na Rais Samia, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na viongozi wote wa serikali kutufanya wazee kupata heshima tunayoistahili," anasema na kuongeza:

"Sisi wazee wa Handeni, tunaamini kwamba utetezi huu utaendelezwa na Rais wetu mpendwa Samia, tuliyekabidhiwa na Mwenyezi Mungu kuiongoza Tanzania baada ya kifo cha Magufuli."

Pia, mzee mwenza Mama Bonaventura, anasema ujasiri alioyokuwa nayo Dk. Magufuli katika uhai wake, uliwezesha mengi, zikiwamo sheria za kutengwa asilimia 10 ya mapato ya ndani katika serikali za mitaa, kutoa mkopo usiokuwa na riba kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Hivi sasa wanawake tunanufaika kupitia mikopo ya asilimia 10 inayoelekezwa kwetu (asilimia nne), kwa vijana (asilimia nne) na watu wenye ulemavu (asilimia mbili). Mikopo imetusaidia kujenga uchumi na kuzifanya familia zetu kusimama," anasema.

Ni tukio lililokusanya maelfu ya wakazi Handeni, ikiwa hali inayodhihirisha kwamba dunia itaendelea kutambua umoja na mshikamano uliopo Tanzania, ikiwamo katika nyakati za matukio yanayogusa ubinadamu zaidi.

***Mwandishi wa makala haya ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga. Anapatikana kwa simu namba: +255 754 691540***



# PLAJC yawashauri Watanzania subira

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KITUO cha Amani, Haki na Msaada wa Kisheria Tanzania (PLAJC) kimewataka Watanzania kuwa na subira, ikiwamo kuacha kusikiliza maneno ya mitandaoni badala yake waliombee amani taifa kutokana na msiba mkubwa wa kumpoteza Rais Dk. John Magufuli.

Rais Magufuli, alifariki dunia Machi 17 katika Hospitali ya Mzena jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na uongozi wa kituo hicho na kusainiwa na Jaruo Karebe, inauomba uongozi wa Rais Samia Hassan Suluhu kuendelea na mapambano ya ujenzi wa taifa ili kutekeleza maono ya hayati Rais Dk. Magufuli ya kujenga Tanzania imara ya kiuchumi na yenye amani.

Taarifa ya PLAJC katika salamu zao kwa Watanzania, inasema katika kipindi cha uhai wake, Rais Magufuli alionyesha upeo wa juu wakizalendo kwa nchi yake na kwa wananchi wanyonge kwa kutetea haki zao za msingi kwa kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati ikiwamo vituo vya afya, shule, hospitali, barabara na reli.

"Tunaomba haya mapambano yaendelezwe ili tutimize ndoto ya Hayati Rais Dk. Magufuli ya kuwa Tanzania mpya yenye uchumi," ilieleza taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilisema kwamba Hayati Rais Magufuli alionyesha dhamira safi ya kutumikia wananchi na kuwatoa katika lindi la umaskini kwa kuwa na mikakati madhubuti ya kuinua uchumi ambayo alimsimamia kwa weledi mkubwa.

Taarifa hiyo ilisema Hayati Dk. Rais Magufuli alishiriki katika mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi mambo ambayo yalikuwa yanachochea uharibifu wa haki mbalimbali za wananchi.

Alisema vitu alivyovifanya Hayati Dk. John Magufuli vinapaswa kuenziwa kwa kuendelezwa ili Watanzania waendelee kufurahia matunda ya uongozi wake.

**"Tunaomba haya mapambano yaendelezwe ili tutimize ndoto ya Hayati Rais Dk. Magufuli ya kuwa Tanzania mpya yenye uchumi," ilieleza taarifa hiyo.**

# SIDO yawapa mbinu za uzalishaji wajasiriamali

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SHIRIKA la Viwanda Vidogo (SIDO) mkoani Dodoma, limewataka wajasiriamali kujenga utaratibu wa kuzalisha bidhaa endelevu badala ya kusubiri maonyesho ya kitaifa na kimataifa, ili kupanua wigo wa biashara zao pamoja na soko.

Hayo yalibainishwa na ofisa wa shirika hilo Mkoa wa Dodoma, Nyangusi Mollel, wakati akielezea umuhimu wa utengenezaji wa bidhaa bora za lishe ambazo hutengenezwa na wajasiriamali.

Alisema wajasiriamali wanatakiwa kuweka utaratibu wa kuwa na bidhaa endelevu, jambo ambalo litawasaidia kupata soko kutoka maeneo tofauti pale bidhaa zinapohitajika.

"Kwenye uzalishaji wa bidhaa angalia soko linahitaji nini pia jifunze kutoka kwa wenzako wana nini cha peke yako kuhusu wewe," alisema Mollel.

Alisema shirika limekuwa likitoa mafunzo ya usindikaji wa vyakula, utengenezaji wa bidhaa za ngozi, utengenezaji sabuni, mafuta na bidhaa mbalimbali, hivyo nao wanatakiwa kuwa wabunifu ili waendane na uhalisia wa soko.

Hata hivyo, aliwataka wajasiriamali kuchangamkia fursa za kupata mafunzo ili kuboresha biashara na kupata mbinu za kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Alifafanua kuwa mjasiriamali anapaswa kuwa na mpango kazi na awe makini nao na ajue bidhaa zake anapeleka kwenye soko gani.

Naye Ofisa Miradi wa SIDO Mkoa wa Dodoma, Stephano Ndunguru, aliwataka wajasiriamali kuwa na utaratibu wa kutafuta taarifa mpya ambazo zitawasaidia kujenga biashara zao.

Alisema SIDO inahitaji kuona wajasiriamali wanatumia fursa kusonga mbele na bidhaa wanazotengeneza, jambo ambalo litawasaidia kufika mbali katika kile wanachotengeneza kupeleka sokoni.

Mjasiriamali Isack Mota, aliwataka wajasiriamali kuungana ili kufanya kazi kwa pamoja ikiwamo kuunda vikundi ambavyo vitasaidia kupata mikopo kutoka taasisi za serikali au binafsi.

Alisema wakati huu Jiji la Dodoma lina watu wengi kutokana na ujio wa serikali, ni muhimu kujipanga kuzalisha bidhaa nyingi zenye ubora ili kuchangamkia fursa ya kuuza bidhaa kwa wingi.

Alisema bidhaa zinapokuwa na ubora zinamhakikishia mjasiriamali soko la uhakika katika mafunzo hayo washiriki walijifunza kwa nadharia na vitendo usindikaji wa mvinyo, pilipili, unga wa lishe, ukaushaji wa mboga na utengenezaji wa keki.



Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, akisaini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, jijini Dodoma juzi. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Mutamwega Mgaywa ammwagia sifa JPM

**Na Ibrahim Josph, DODOMA**

ALIYEKUWA mgombea urais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Mutamwega Mgaywa amesema Hayati Rais Dk. John Magufuli, alikuwa mtu mwenye kusimamia maamuzi yenye maslahi ya nchi na kufanya kazi kwa vitendo.

Mgaywa alisema hayo wakati alipozungumza na Nipashe jijini hapa baada ya kusaini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Magufuli.

Alisema tangu alipomfahamu Dk. Magufuli mwaka1995 walipoingia wote Bungeni anamkumbuka kwa maamuzi yake sahihi na yenye kusimamia maslahi sahihi ya nchi bila kubagua.

"Dk. Magufuli alikuwa ni Rais aliyejitoa kwa ajili ya wananchi na alitekeleza jambo sahihi kwa wakati lenye lengo la kuwanufaisha watu wake bila woga wowote kwa vitendo," alisema.

Alisema kuanzia alipokuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na baadaye kufanyakazi kwenye wizara tofauti akiwa waziri alifanyakazi kwa weledi na hakuwa mwoga katika kutekeleza jambo ambalo alikuwa akiamini kuwa linamaslahi ya nchi.

Kadhalika, alisema Hayati Dk. Magufuli alifanikiwa kuinua uchumi wa nchi kwa sababu aliwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu muhimu ambayo iliiwezesha kuingia kwenye uchumi wa kati.

Alibainisha kuwa yeye alifahamiana na Hayati Rais Magufuli tangu mwaka 1995 wakiwa kwenye usafiri wa ndege kutoka Mwanza kuelekea Dar es Salaam kuapishwa baada ya kuchaguliwa.

Alisema baada ya kuapishwa waliendelea kuwa na uhusiano mzuri wa kikazi bila kujali kuwa Mgaywa alikuwa mbunge kutoka chama cha upinzani cha TLP.

Hata hivyo, alisema akiwa bungeni aliwahi kuomba ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa baadhi ya maeneo ya jimbo lake pamoja na kuunganisha Mkoa wa Mwanza na Mara na serikali ilizifanyia kazi.

Aliongeza kuwa mwaka 2020, aligombea urais pamoja na wenzake kwenye uchaguzi Mkuu Oktoba, lakini kura zake hazikutosha na wananchi wakamchagua Dk. Magufuli.

"Pamoja na na tofauti zetu za kisiasa, Dk. Magufuli hakuacha kutushirikisha baadhi ya mambo ya kitaifa, kwa sababu nafasi ya urais ilihitaji mtu moja tusingeweza kuwa wote marais," alisema.

"Nipo hapa Dodoma nilikuja kwenye mazishi yake kitaifa, lakini natarajia kusafiri kwenda Chato kijijini kwake kushirikiana na Watanzania wenzangu kumhifadhi mwenzetu huyu aliyetangulia mbele za haki," alisema.

Aidha, alisema yeye binafsi ataendelea kumuunga mkono Rais mpya Samia Suluhu Hassan, kwa sababu anaona kuwa ni mtu anayefaa kuwa kiongozi wa nchi kutokana na uchapazi na aliyekuwa karibu na Dk. Magufuli.

"Dk. Magufuli alikuwa akimtuma Samia kumwakilisha kwenye mikutano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi hiyo tu ilitosha kuonyesha kuwa alikuwa akimwamini na akimwandaa kuwa kiongozi wa mkuu wa nchi," alisema.



HABARI MBEYA

# Wenye ulemavu wamkumbuka JPM kwa mikopo

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WATU wenye ulemavu mkoani Mbeya wameeleza masikitiko yao kutokana na kifo cha Rais Dk. John Magufuli kwa kuwa aliwathamini katika mikopo ya asilimia mbili ambayo inatokana na mapato ya ndani ya halmashauri nchini.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Mbeya, Jimmy Mwambepo, alisema, Hayati Dk. Magufuli, alikuwa ni Rais aliyewathamini wanyonge ndio maana alihakikisha sheria inatungwa ili halmashauri zitoe mikopo kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Alisema mikopo hiyo ilisaidia kundi hilo kujikwamua kiuchumi kwa kuwa walifungua na kuanzisha miradi ya maendeleo na kuondokana na utegemezi.

"Kifupi Hayati Magufuli alituthamini, alikuwa kiongozi kweli wa wanyonge kwa matendo maana alisimamia utolewaji wa mikopo kwa kuzielekeza halmashauri zote zinatelekeza agizo hilo, naomba viongozi serikalini kusimamia na kuyeanzi mema yote aliyoyaasisi," alisema mmoja wa viongozi hao.

Alisema Hayati Dk. Magufuli alijitahidi kutengeneza miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu na kuagiza taasisi mbalimbali za umma na binafsi ili watu hao wasipate shida kutembea au kupata huduma na kukomesha mauaji ya watu wenye ualbino.

Mwenyekiti wa Idara ya Wanawake wenye Ulemavu mkoa, Bahati Bukubilo, alisema Hayati Magufuli enzi za utawala wake, aliwapatiwa uwakilishi kwenye ngazi mbalimbali za uongozi serikalini na kuchangia kundi hilo kuwa watetezi na kuendelea kuthaminika kutokana na shughuli mbalimbali wanazozifanya.

Mwakilishi wa wenye ulemavu, Siza Mwahula, alimwomba Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kusimamia aliyoyalenga kuyatekeleza katika kipindi cha utawala wake bila kusahau kuwapigania wenye ulemavu katika mambo mbalimbali ili kuhakikisha wanapiga hatua kiuchumi.

Alisema wana imani kubwa kwa Rais Samia kuendeleza mambo yote ambayo yalikuwa ni ndoto ya mtangulizi wake katika kuhakikisha anajenga uchumi imara ikiwamo upatikanaji wa mikopo kwa makundi hayo.



Baadhi ya maofisa wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), wakikagua chanzo cha maji cha Nzovwe juzi, ambacho ni miongoni mwa vyanzo 16 vya maji vinavyohudumia Jiji la Mbeya na Mji Mdogo wa Mbalizi. PICHA: NEBART MSOKWA

# Wasomi kutumia mil. 400/ za mkopo kujitegemea

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

VIJANA wasomi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamesema kiasi cha Sh. milioni 400 kilichotengwa kwa ajili ya kukopeshwa kitasaidia kuachana na utegemezi na kufanya shughuli zitakazosaidia kuanzisha familia zao na kuzihudumia.

Mhitimu wa chuo kikuu, Kalole Mnasi, alisema kutokana na uhaba wa ajira na ukosefu wa mitaji waliamua kujitolea kufundisha shule mbalimbali ndani ya wilaya hiyo ili ujuzi walioupata vyuoni usipotee.

Kutokana na jitihada hizo, Wilaya ya Mbeya ilifurahishwa na vijana hao na kuwahamasisha kujiunga kwenye vikundi ili kupatiwa mtaji utakaowawezesha kuanzisha biashara zao na kuajiri wengi ili kuendesha maisha yao.

"Kundi langu tulijitolea vijana 33 kufundisha shule mbalimbali za sekondari ili kuwasaidia wadogo zao kufanya vizuri kwenye mitihani, lakini kuziba pengo la uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi," alisema Mnasi.

Akizungumza na vijana waliomaliza elimu ya juu wasiokuwa na ajira rasmi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Stephen Katemba, alisema fedha hizo zilitolewa na Hayati Dk. Magufuli ili kuwawezesha vijana kujikwamua na umaskini kupitia shughuli watakazozianzisha.

Aliwahakikishia atasimamia mchakato wa fedha hizo kutolewa ili waanze mara moja kufanya shughuli zao za ujasiriamali na kuleta mabadiliko kwenye maisha yao na kuwasaidia wanaowategemea.

Pia aliwataka vijana wasomi kubuni miradi ikiwamo kuanzisha kiwanda cha kufyatua tofali, ufugaji wa kuku na utengenezaji wa vyakula vya mifugo na kuwahakikishia kuwa halmashauri hiyo itakuwa mteja mkubwa wa bidhaa.

Ofisa vijana wa Wilaya ya Mbeya, Consolata Kyando, alisema vijana wengi hawana ajira rasmi na kwamba mikopo watakayopatiwa wakafanye shughuli iliyokusudiwa ili waweze kujikwamua na umaskini.

# Waahidi kujitoa kukamilisha ujenzi madarasa

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANANCHI wa Kata ya Iganzo, wamesema wataendelea kujitoa kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kumaliza kabisa tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari ya kata hiyo. Wakizungumza na Nipashe juzi wananchi hao walisema, licha ya kuwa kwenye maombolezo ya Hayati Dk. John Magufuli, wataendelea kuenzi uzalendo na kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema Hayati Dk. Magufuli aliwahamasisha wananchi kujitolea nguvu kazi ili kuboresha miundombinu ya elimu huku yeye akitoa fursa ya watoto kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari kutokulipa ada.

Miongoni mwa wananchi hao, Butusyo Moses, alisema hadi sasa vyumba sita vilivyohitajika kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kuanza shule vimekamilika na wanaendelea kukusanya nguvu kuanza ujenzi wa vyumba vingine ili kuondoa tatizo la uhaba wa vyumba hivyo.

Akiongea na wananchi hao Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, alisema jumla ya Sh. milioni 69 zimetolewa kukamilisha ujenzi wa vyumba sita. Alisema fedha hizo zimeongeza nguvu kwenye ujenzi huku wadau mbalimbali wakiunga mkono ukamilishaji wa vyumba hivyo. Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, hivi karibuni alitoa mifuko 200 ya saruji kwa ajili ya ujenzi huo ikiwa ni sehemu ya mchango wa Mbunge katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema ataendelea kuchangia mahitaji katika shule hiyo ili kuhakikisha watoto wanasoma kwenye mazingira mazuri na ya utulivu kama sera ya elimu ilivyoelekeza.

**'Hayati Dk. Magufuli aliwahamasisha wananchi kujitolea nguvu kazi ili kuboresha miundombinu ya elimu'**

## Washauriwa kutowafungia watoto wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JAMII imeshauriwa kuwatoa nje na kutowafungia ndani watu wenye ulemavu ili kupata haki zao za msingi kama wanavyopata watu wengine.

Ushauri huo umetolewa na Msaidizi Mkurugenzi Masuala Mtambuka wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati, Makame Hassan Mussa, wakati alipofanya ziara ya kuwatembelea watu wenye ulemavu wa shehia nne zilizokuwamo katika wilaya hiyo.

Alisema kuwa ni vyema jamii ikafahamu kuwa watu wenye ulemavu wana haki sawa na wengine na ndio maana baraza hilo linachukua jitihada za kuwatembelea na kuwapatia msaada wa vifaa mbalimbali.

"Nakuombeni wananchi ambao ndani ya familia zenu mnaishi na watu wenye ulemavu, ni vyema mkawatoa ili wapate haki zao, kuwafungia ndani sio vizuri na itakuwa mnawafanyia vitendo vya udhalilishaji," alisema.

Hassan aliwataka wanafamilia wanaoishi na watu wenye ulemavu kuvitunza viti walivyopewa vijana hao ili vidumu katika matumizi yao ya kila siku.

Aliipongeza Taasisi ya 'Nyota Foundation' kwa kuona umuhimu wa kutoa msaada huo kwa watu wenye ulemavu na kuwaomba usiwe mwisho bali wawe wanasaidia kwa kila kunapokuwa na uhitaji.

Naye Katibu wa Taasisi ya Nyota Foundation ya Dar es Salaam, Zainab Mvungi, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuwasaidia watu wenye ulemavu ambao wana nafasi kubwa katika jamii na wanahitaji kuenziwa.

Alisema anaamini msaada wa viti mwendo utawasaidia katika mambo mbalimbali ikiwamo kufika safari zao pamoja na shughuli wanazofanya zikiwamo za kujiajiri.

Mzazi wa mmoja wa watoto waliopatiwa msaada huo, Tatu Khamis, kutoka shehia ya Pagali, aliishukuru taasisi hiyo na Baraza la Mji Kati kwa msaada waliowapatia ambao utarahisisha maisha yao.

Alisema msaada walioupata umewapa faraja na matumaini mapya katika maisha yao na kwamba watajitahidi kuutumia kwa kuutunza ili watoto wao waweze kufaidika nao zaidi.

"Naamini msaada huo utatusaidia katika mahitaji mbalimbali na naahidi mimi na wazee wenzangu, tutatumia msaada waliopatiwa watoto wetu na kuutunza kwa mahitaji ya watoto wetu," alisema.

Katika hafla hiyo, taasisi hiyo, ilitoa viti mwendo vya watu wenye ulemavu vyenye thamani ya Sh. 350,000 vimetolewa na Taasisi ya Nyota, msaada ambao unatajwa kutoa nafuu kwa watoto na walezi wa watoto hao katika maisha yao ya kila siku.

# SACCOS yakumbushwa utaratibu utunzaji fedha

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha Kuweka na Kukopa cha Watanga (Watanga SACCOS), kimetakiwa kuweka utaratibu mzuri wa utunzaji wa taarifa zake ikiwamo mapato na matumizi ambayo ndio nguvu kubwa ya kufanya uwekezaji na kujiendesha kibiashara.

Hayo yalielezwa juzi na Ofisa Mwandamizi kutoka Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ), Muhammed Ismail, wakati akifungua mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika mjini hapa.

Alisema kutunza mahesabu yao kutawasaidia wao na serikali kuu kutatua changamoto za kijamii hasa za kiuchumi na kwamba jukumu la utunzaji wa mahesabu haliepukiki.

Aliwataka kufanya shughuli za maendeleo ili kujiendesha kibiashara na kujikwamua kiuchumi hasa ikizingatiwa kuwa wanachama wengi ni wanawake na ndio walezi wakuu wa familia.

"Ili kutimiza malengo yenu muwekeze katika miradi mikubwa ambayo itakua na faida kubwa ambapo zipo SACCOS zingine zimefanya uwekezaji mkubwa hivyo kuiga mfano huo," alisema.

Akisoma risala kwa niaba ya wanachama, Mariyam Suma alisema, umoja wao una malengo mengi ikiwamo kutoa huduma za kifedha kwa wanachama wake ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya kiuchumi na kijamii na kuondokana na umaskini wa kipato kwa wanachama.

Alisema wanakusudia kuimarisha miradi mikubwa ya kiuchumi ili chama chao kipate maendeleo endelevu mapema iwezekanavyo.

Alisema vikwazo wanavyopambana navyo katika kufikia malengo yao ni kuwa na utitiri wa kodi, kukosa fursa za mafunzo na upatikanaji wa vitendea kazi bora.

Pia alisema masharti magumu ya kupata mikopo kutoka katika taasisi kubwa za kifedha ikizingatiwa kuwa SACCOS zinajitahidi kuwawezesha wajasiriamali wadogo kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu.

"Moja ya masharti hayo magumu ni kupewa muda mfupi wa kufanya marejesho ya mkopo na mkopo kuwa na riba kubwa," alisema.

Alisema kuwa licha ya matatizo hayo, SACCOS yao imepata maendeleo ikiwamo kuijali jamii kwa kusaidia mambo mbalimbali ikiwamo kuchangia damu, kusafisha mazingira na kutoa misaada kwa wanafunzi.




Ofisa Mwandamizi wa Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ), Muhammed Ismail (kushoto), akifungua mkutano mkuu wa chama cha kuweka na kukopa cha Watanga, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ujenzi madarasa wakomboa wanafunzi kukaa chini ya miti

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KUMALIZIKA kwa ujenzi wa madarasa mapya ya Shule ya Kama, Wilaya ya Magharib A Unguja, kutapunguza tatizo la wanafunzi kukaa chini ya miti wakati wakifundishwa.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ya Kama, Khamis Omar Khamis, wakati akizungumza baada ya kukabidhiwa kwa vifaa mbalimbali vya ujenzi ikiwamo matofali na saruji vilivyotolewa na Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini Machano Othman Said.

Alisema kwa mwaka huu wanafunzi wapya walioandikishwa shuleni hapo ni 329 na madarasa yaliyopo ni machache na kulazimika baadhi ya wanafunzi kuwaweka chini ya mti.

Alisema kukabidhiwa kwa vifaa hivyo kutasaidia kuendeleza ujenzi huo shuleni hapo na kuwawezesha wanafunzi kupata elimu wakiwa ndani ya madarasa.

"Mvua za masika karibu zitaanza kunyesha hivyo tunahofu kubwa kwa wanafunzi wetu maana wanaokaa chini ya mti watakosa sehemu ya kupata elimu," alisema mwalimu huyo.

Pia aliwataka wazazi na walezi kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni kwa sababu badhi ya wanafunzi hawafiki shule badala yake wanajishughulisha na biashara ndogo.

Alisema hivi sasa ni msimu wa tunda la zambarau na wanafunzi wengi wamejikita huko kwa ajili ya biashara huku wazazi wao wakijua kuwa wapo shuleni.

"Kipindi kama hiki cha msimu wa zambarau utoro ni mkubwa shuleni hapa watoto hawaji shule hasa wanafunzi wa kiume," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othaman Said, alisema vifaa alivyovitoa ni miongoni mwa ahadi alizoahidi yeye na mbunge wa jimbo hilo wakati walipokua wakiomba kura kipindi cha kampeni.

"Nakumbuka nilifika shuleni hapa na walimu walinieleza masikitiko yao kuwa idadi ya wanafunzi shuleni hapo inaongezeka, lakini changamoto ni uhaba wa madarasa na hawana pakuwaweka hivyo mimi na mbunge wangu tumeamua kuanza kutekeleza ahadi tuliyoahidi," alisema.

Machano aliwataka walimu wa shule hiyo kuvitunza vifaa hivyo na kusimamia ujenzi wa madarasa ili kuepusha udanganyifu na ubadhirifu katika ujenzi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## BEACH HOUSE FOR RENT

Beach House for rent in OSTERBAY DAR ES SALAAM with swimming pool. For more information contact: 0689 879 642.

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

## UPOTEVU WA KADI YA GARI

**JOSEPH MWITA MWIKWABE** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 569 BKB TOYOTA COROLLA.** Chassis namba AE1116159474. Yeyote atakayeionа atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/156616/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.81/2021**

Ombi la **REHEMA WILLIAM JASSEDA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **WILLIAM SAMWEL JASSEDA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 31//03/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 23/3/2021**

Tarehe 23/3/2021
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA KINONDONI**
**SHAURI LAM MAOMBI NA.132 YA MWAKA 2020**
**TUJIJENGE TANZANIA LIMITED MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA.....MJIBU MAOMBI**
**REHEMA JUMA MOHAMED**
**KWA**
**REHEMA JUMA MOHAMED**
**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii,kwahiyo unahitajika kuhudhuria mahakama hii binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya JUMATATU tarehe 12 mwezi wa 4 mwaka 2021 saa 2:00 asubuhi
Kwa mujibu wa maombihayo na kwakuwa siku hiyo ni siku ya hukumu shauri hilo ni lazima uhudhurie
**ANGALIZO.**
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitika kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 23 mwezi wa 3 mwaka 2021

Hakimu Mkazi
Mahakama Ya Wilaya
Kinondoni

**GSP AUCTION MART**

## TAARIFA KWA UMMA

TANGAZO LILITOKA KATIKA GAZETI LA NIPASHE LA TAREHE KUMI NA MOJA MARCH MNADA AMBAO ULIKUA UFANYIKE TAREHE 26/03/2021 SIKU YA IJUMAA UTAFANYIKA TAREHE 29/03/2021 SIKU YA JUMATATU SABABU YA MABADILIKO YA TAREHE YA MNADA NI KUTOKANA NA MSIBA WA KITAIFA WA HAYATI JOHN POMBE MAGUFULI.

**GSP AUCTION MART**
**+255 654 922 892,**
**+255 687 638 679.**

## UPOTEVU WA KADI YA GARI

Ndugu **MWAJUMA MWENGUO RASHID** amepotelewa na kadi yake ya gari
Aina yake **(TOYOTA PASSO)** Yenye usajili namba **T 967 DDX ( CHASSIS NO ONC100095800)**
KWA YOYOTE ATAKAE ONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.RB NO.MOR/MOR/RB/163432/2021

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.63/2021**

Ombi la JOHA JUMANNE OMARY kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu THADEY ABED MGAYA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 08/04/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 4/03/2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Watatu wauawa kwa bomu Kenya

**Mandera,** KENYA

TAKRIBANI watu watatu wameuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa wakati basi walilokuwa wakisafiria, lilipopigwa na bomu lililotegwa katika barabara ya Arabia katika Kaunti ya Mandera nchini Kenya.

Basi hilo lilikuwa njiani kuelekea katika mji wa Mandera ulioopo mpakani mwa Kenya na Somalia jana, lilipopigwa na kilipuzi kilichotegwa.

Walioshuhudia tukio hilo walisema basi hilo liliharibika vibaya baada ya kulipuka.

Picha zilizochukuliwa kutoka kwenye eneo la tukio zilionyesha basi hilo likiwa limepasuka vipande huku waathiriwa wakiwa wamelala chini.

Polisi ilisema kuwa inahofia idadi ya majeruhi kuongezeka. Gavana wa Mandera, Ali Roba, alithibitisha idadi ya vifo.

Shambulio hilo linakuja siku moja, baada ya maofisa wa usalama kuzima jaribio la wanamgambo wa Al-Shabaab, la kushambulia kambi ya polisi iliyopo katika eneo la Lafey, katika Kaunti ya Mandera.

Inaaminiwa kuwa kundi hilo ndilo lililohusika na shambulio.

BBC



Mwandishi wa habari wa Shirika la Associated Press (AP), Thein Zaw (katikati), akiwa na familia yake akipunga mkono nje ya gereza la Insein baada ya kuachiliwa kutoka kizuizini jana. Zaw, alikamatwa mwezi uliopita wakati akiripoti kuhusu maandamano dhidi ya mapinduzi nchini Myanmar. **PICHA: APAFP)**

# Sassou-Nguesso ashinda urais

**Brazzaville,** CONGO

RAIS wa Congo-Brazzaville, Denis Sassou-Nguesso, amechaguliwa tena kuwa rais wa nchi hiyo kwa asilimia 88.57 ya kura kwa kipindi cha miaka mitano, kulingana na matokeo rasmi ya awali ya Tume ya Uchaguzi, yaliyotangazwa na Waziri wa Mambo ya Ndani.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Raymond Mboulou, juzi, alisiri alisoma matokeo kutoka wilaya moja kwa moja kwenye runinga ya serikali.

Saa mbili za kutangazwa kwa matokeo hayo, ilikuwa mkusanyiko wa ushindi kwa rais anayemaliza muda wake, ambaye kwa upande wake takwimu za tume ya uchaguzi zinatoa ushindi mkubwa.

Denis Sassou-Nguesso, mwenye umri wa miaka 77, pamoja na miaka 37 akiwa madarakani kama rais wa nchi, alishinda kila maeneo. Katika ngazi ya kitaifa, tume ya uchaguzi inampa ushindi wa asilimia 88.57 ya kura, ambayo ni zaidi ya kura 700,000 za ziada ikilinganishwa na mwaka 2016, wakati alipopata asilimia 60.19 ya kura.

Miongoni mwa wagombea wengine sita katika kinyang'anyiro hicho ni Guy-Brice Parfait Kolélas aliyefariki Jumapili wiki iliyopita, kwa ugonjwa wa Covid-19 mara tu baada ya kuwasili nchini Ufaransa.

Alihesabiwa kupata kura nyingi, baada ya kupata asilimia 7.8. kwa upande wa upinzani, Waziri wa zamani Mathias Dzon alipata asilimia 1.90 ya kura na wagombea wengine wako chini ya asilimia moja ya kura.

Kiwango rasmi cha ushiriki kilifikia asilimia 67.55.

Wapinzani tayari wametangaza kwamba watawasilisha malalamiko yao mbele ya mahakama ya Katiba.

Washirika wa karibu wa Guy-Brice Parfait Kolélas wamelaani udanganyifu mkubwa wa kura.

Mathias Dzon, kwa upande wake, alibaini kwamba uchaguzi huo haueleweki, huku wakiwa na siku tatu kuwasilisha malalamiko yao kwenye mahakama hiyo.

RFI

## Abiy: Jeshi la Eritrea liliingia Tigray

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, amethibitisha kwamba wanajeshi kutoka nchi jirani ya Eritrea, waliingia katika jimbo la Kaskazini la Tigray wakati wa vita vya miezi mitano.

Kauli hiyo ni mara ya kwanza, kutolewa na waziri mkuu huyo, jana.

Abiy alisema wanajeshi wa Eritrea walivuka mpaka na kuingia Tigray kwa sababu walikuwa na wasiwasi wa kushambuliwa na vikosi vya Tigray na waliahidi kuondoka baada ya jeshi la Ethiopia kuwa na uwezo wa kuudhibiti mpaka. Katika hotuba yake mbele ya bunge mjini, Addis Ababa Abiy Ahmed alisema ripoti zinaonyesha mauaji makubwa yamefanyika katika jimbo la Tigray.

Aliahidi kwamba wanajeshi waliowabaka wanawake au waliohusika na uhalifu mwingine wa kivita watachukuliwa hatua za kisheria.

Ingawa pia alisema chama cha TPLF kimeeneza propaganda juu ya matukio ya jimbo hilo.

Kadhalika alisema kwamba nchi yake haitaki kuingia vitani na Sudan.

Tangazo hilo alilitoa wakati kukiwako mivutano baina na Sudan, juu ya eneo lililoko kwenye mpaka baina ya nchi hizo mbili unaochochea hofu ya kuzuka vita kamili.

DW

## 18 waachiliwa na vikosi Uganda

**Kampala,** UGANDA

WANAUME 18 walioaminika kushikiliwa na vikosi vya usalama vya Uganda, wameachiwa na kuruhusiwa kurejea kwenye kijiji walichotoka.

Watu hao waliokamatwa wakati wa uchaguzi mwezi Januari, walisema hawajui walikuwa wakishikiliwa wapi.

Baada ya kuachiwa kwao , baadhi yao wameiambia BBC kuwa walitupwa kwenye idara ya usalama katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kyotera, Kusini mwa Jiji la Kampala, Jumatatu usiku.

Mmoja wao, John Kiwanuka, alidhaniwa kuwa amekufa, baada ya kupatikana damu nyingi kwenye chumba chake cha kulala baada ya kukamatwa mwezi Januari.

Serikali ilikiri kuwa inawashikilia watu 200, kwa shutuma za kushiriki maandamano au kwa madai ya kukutwa na mali za jeshi.

Lakini takwimu za serikali hazihusishi kundi la wanaume 18 walioachiwa.

BBC



# ARSENAL

## WAJIPANGA KUMBAKISHA ODEGAARD

**LONDON, England**

ARSENAL inaamini kuwa, Martin Odegaard, ambaye anaichezea timu hiyo kwa mkopo kutoka Real Madrid anaweza kuongeza mkataba wa kuendelea kuwapo hapo Emirates, kwa mujibu wa Sky News.

Kiungo huyo ambaye alijiunga na 'Washikabunduki' hao wa London Januari, mwaka huu kwa mkataba wa mkopo wa muda mfupi, ameonekana kuwa kwenye kiwango bora akiwa na kikosi hicho cha Mikel Arteta ambacho amekifungia mabao mawili kwenye michezo 12.

Odegaard alionyesha uwezo mkubwa kwenye mchezo uliopita wa Ligi Kuu England ambao Arsenal ilitoka nyuma na kwenda sare ya mabao 3-3 dhidi ya 'Wagonga Nyundo' wa London West Ham.

Kwa mujibu wa ripoti raia huyo wa Norway, anaweza kuendelea kuwapo Arsenal hata baada ya mkataba wake wa mkopo kumalizika mwishoni mwa msimu.

Ripoti kutoka Hispania, zinaeleza kuwa Real Madrid inaweza kumwachia nyota huyo, lakini kwa dau lisilopungua pauni milioni 51.

Na iwapo Arsenal watashindwa kufikia dau hilo namna pekee ya kumbakisha kiungo huyo ni kuongeza mkataba wake wa mkopo.

## RODRIGUEZ FITI KUREJEA DIMBANI EVERTON



**LIVERPOOL, England**

JAMES Rodriguez amepanga tarehe ya kurejea dimbani pale Everton kuwa ni Aprili 3, mwaka huu baada ya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu kutokana na kuwa majeruhi.

Raia huyo wa Colombia kwa mara ya mwisho alicheza katika kikosi hicho cha kocha Carlo Ancelotti katika mchezo wa Februari 20 dhidi ya Liverpool.

Alikuwa akisumbuliwa na jeraha dogo, lakini hajaonekana tangu aanze kukabiliana na tatizo hilo.

Alipoulizwa na waandishi wa habari ni lini anatarajia kurejea katika kikosi cha Everton, James alisema: "Nitacheza tena katika mchezo wa Aprili 3 nadhani. Nipo vizuri na ninataka kucheza tena."

Kwa mara ya mwisho James kuwachezea Toffees hao ni wakati wa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Liverpool katika mchezo ambao alikamilisha dakika 62 kwenye mechi hiyo.

Walipata ushindi pia kwenye mchezo uliofuata katika Ligi Kuu dhidi ya Southampton na West Brown ambayo iliwapa tumaini la kushiriki katika michuano ya Ulaya.

Everton watarejea dimbani baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa ambapo watacheza na Crystal Palace Aprili 5, mwaka huu.



## IBRAHIMOVIC: HAIKUWA RAHISI KURUDI SWEDEN

**LONDON, England**

ZLATAN Ibrahimovic alidondosha machozi wakati akihojiwa na vyombo vya habari Jumatatu baada ya kuelezea kurejea kwake timu ya Taifa ya Sweden kuwa halikuwa jambo rahisi kwa familia yake.

Straika huyo wa AC Milan ameitwa tena katika kikosi cha Sweden chini ya kocha, Janne Andersson kwa ajili ya kujiandaa na michuano ya kufuzu Kombe la Dunia kwa kuwavaa Kosovo na Georgia.

Alikuwa akisherehekea kuitwa kwake kwa mara ya kwanza katika timu ya taifa baada ya kupita miaka mitano kwa kuweka posti ya picha katika akaunti yake ya Twitter na ujumbe uliyosomeka: "Kurejea kwa Mungu."

Ibrahimovic ambaye Oktoba atafikisha umri wa miaka 40, ndiye mfungaji wa wakati wote wa Sweden akiwa na mabao 62 na mara ya mwisho alifunga dhidi ya Denmark mwaka 2015.

Akizungumza na waandishi wa habari Ibrahimovic alisema ilikuwa ni ngumu kuiacha familia yake na kujiunga na timu ya taifa.

"Nina mtoto wangu wa kiume ambaye kiukweli alikuwa analia nilipomuacha. Lakini sawa," alisema kabla ya kububujikwa na machozi.

"Hili jambo la kwenda mbali na familia yangu siyo jambo rahisi, kama una watoto wawili ambao wanalia kila wakati unapowaacha, ni ngumu kidogo, mimi ni binadamu."

## HABARI MICHEZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

# TANZIA



PUMZIKA KWA AMANI

**1959 - 2021**

DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI

MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI, TUNAUNGANA NA WATANZANIA WOTE KUOMBOLEZA MSIBA WA ALIYEKUWA RAIS WA AWAMU YA TANO HAYATI .DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI ULIOTOKEA TAREHE 17/3/2021 KATIKA HOSPITALI YA MZENA MKOANI DAR ES SALAAM

TUTAENDELEA KUMUENZI KWA UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU NCHINI BWANA AMETOA, BWANA AMETWAA, JINA LA BWANA LIHIMIDIWE.





## KWA UFUPI

### KANE ATAKIWA MADRID

REAL Madrid inafikiria kumsajili straika wa Tottenham na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27. (**SER Deportivos**)

### RODRIGUEZ AWANIWA ARSENAL

ARSENAL wanataka kumsajili kiungo mkabaji wa Real Betis na Argentina, Guido Rodriguez, mwenye umri wamiaka 26. (**Mundo Deportivo via Metro**)

### NACHO AKODOLEWA MACHO

LIVERPOOL, Juventus na AS Roma zinafuatilia hali ya Nacho kule Real Madrid, huku beki huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 31, akiwa anaingia mwaka wake wa mwisho kwenye mkataba wake. (**AS**)

### KOULIBALY AWANIWA EVERTON

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, anataka kumsajili mlinzi wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, ambaye alimfundisha wakati anainoa klabu hiyo ya Italia. (**Talksport**)

### RONALDO TAYARI KURUDI MADRID

CRISTIANO Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, atakuwa tayari kuondoka Juventus kama Real Madrid wakitoa ofa ya kumsajili nyota huyo wa timu ya Taifa ya Ureno. (**Marca**)

### VAZQUEZ ATAKIWA BAYERN

BAYERN Munich ipo kwenye mazungumzo na mlinzi wa kulia wa Real Madrid, Lucas Vazquez mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake unamalizika Juni. (**AS**)

### RAMOS KUONGEZA MKATABA

MLINZI wa zamani wa Real Madrid, Fernando Hierro ana matumaini beki wa kati, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 34, ataongeza mkataba wake na klabu hiyo. (**Marca**)

### MAN CITY WAMTAKA KAYKY

MANCHESTER City ipo kwenye mazungumzo na Fluminense ili kumsajili kinda wake, Kayky mwenye umri wa miaka 17, ambaye thamani yake inatajwa kuwa pauni milioni 21.5. (**Sun**)

### KOUNDE, TORRES WANUKIA UTD

MANCHESTER United inamkodolea macho nyota wa Sevilla, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22 na mchezaji wa Villarreal, Pau Torres, mwenye umri wa miaka 24, wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja. (**90 min**)

### LLORIS AWINDWA MAN UTD

MANCHESTER United inataka kumsajili golikipa wa Tottenham Hotspur, Hugo Lloris mwenye umri wa miaka 34, ili kuziba nafasi ya David de Gea anayetaka kuondoka. (**L'Equipe via Mail**)

### ZAKARIA ANUKIA MAN CITY

NYOTA wa Uswisi, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 24, ameivutia klabu ya Manchester City, ambayo inamfuatilia kwa karibu kiungo huyo wa Borussia Moncheng-ladbach ili kuziba nafasi ya Fernandinho kipindi cha majira ya joto. (**Sky Sports via Manchester Evening News**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BALE ATANGAZA KURUDI TENA KUKIPIGA MADRID

●●● Sababu kubwa ambayo nilikuja Spurs ni kwamba nilitaka kucheza mpira, nilitaka kuwa sawa, sasa...

**LONDON,** England

GARETH Bale amesisitiza kuwa hana wasiwasi na majaliwa yake ya baadaye na anatarajia kurudi Real Madrid mwishoni mwa msimu huu kama ilivyopangwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 raia wa Wales, alijiunga tena na Tottenham Hotspur kwa mkopo wa msimu mmoja kutoka Madrid Septemba mwaka jana, baada ya kutopata nafasi kule Santiago Bernabeu chini ya kocha Zinedine Zidane.

Mshambuliaji huyo tangu arejee Kaskazini mwa London, amefunga mabao 10 na kusaidia mengine matatu katika mechi 25 kwenye mashindano yote.

Kulikuwa na mazungumzo hivi majuzi juu ya Bale kubaki Spurs baada ya kurudi kwenye kiwango, lakini alilalamikiwa na Jose Mourinho wiki iliyopita na hakushiriki katika ushindi wa Jumapili kule Aston Villa.

Na ikiwa imesalia mwaka mmoja kuendelea na mkataba wake Madrid, straika huyo anaamini atarudi katika mji huo mkuu wa Hispania baada ya kuiwakilisha Wales kwenye mashindano ya Euro 2020 yanayotarajiwa kufanyika Juni mwaka huu.

"Hakuna usumbufu," alisema katika mkutano na waandishi wa habari Jumanne wakati Wales ikijiandaa na mchezo wa ufunguzi wa kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2022 dhidi ya Ubelgiji.

"Sababu kubwa ambayo nilikuja Spurs ni kwamba nilitaka kucheza mpira, nilitaka kuwa sawa. Mpango ulikuwa ni kukaa msimu mmoja tu.

"Baada ya Euro, nimebakiza mwaka na Real Madrid. Mpango wangu ni kurudi tena Madrid."

HABARI MICHEZO

# MTIBWA YAMPASUA KICHWA HITIMANA KUBAKI LIGI KUU

**Na Saada Akida**

HUKU wakiendelea kusuasua katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 24 baada ya kushuka dimbani mara 22, msimu huu, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thierry Hitimana, amesema kazi kubwa aliyonayo kwa sasa ni kuhakikisha timu yake inafanya vizuri na kuepuka kucheza mechi za mchujo (play off) ili kujinasua kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, Hitimana alisema timu yake haijawa kwenye mwendo mzuri, hali ambayo inamuumiza kichwa kuhakikisha wanapambana kwa michezo iliyobaki kupata matokeo chanya.

Alisema kwa sasa yuko likizo na ameenda kwao Rwanda, kabla ya kurejea nchini Aprili Mosi, mwaka huu kuendelea na kazi yake.

"Timu haikuwa na mwenendo mzuri katika ligi, kwa sasa hakuna kingine chakufanya, hatuwezi kuongeza kitu, kilichobaki ni kutumika sana ili tuweze kutoka katika nafasi hiyo mbaya tulipo katika msimamo," alisema Hitimana.

Alisema nafasi ya 14 ambayo wapo kwenye msiamo wa ligi hiyo, ni mbaya kwao hali ambayo inawapasa kupambana kwa mbinu mbalimbali ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi zilizobaki ili kujinasua hapo.

"Napambana kuhakikisha tunapata matokeo katika hizi mechi zilizobaki, ili tusifikie kucheza kwa presha kubwa katika michezo ya 'play off' kama ilivyokuwa msimu uliopita kwa hii timu hii.

"Tumekuwa tukipata matokeo ambayo si rafiki kwetu kwenye mechi zetu, hilo lipo wazi, hivyo ambacho tunafanya kwa sasa ni kupambana kurudi kwenye ubora," alisema Hitimana.

Mtibwa Sugar itakuwa na kibarua kigumu cha kusaka pointi tatu Aprili 6, mwaka huu itakaposhuka katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara.



Beki wa Kati wa Azam FC, Aggrey Morris (Kushoto) na kiungo wa timu hiyo, Khelfi Hamdoun, wakiwa mazoezini juzi kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar itakayopigwa Aprili 6, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Pawassa, Ufukweni waiwinda Burundi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania ya Soka la Ufukweni, Boniface Pawassa, amesema kikosi chake kinaendelea na maandalizi makali ya mchezo wao wa Machi 30 dhidi ya Burundi kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) kwa Soka la Ufukweni zitakazofanyika Mei mwaka huu nchini Senegal.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Pawassa alisema wamerejea mazoezini na kuendelea na maandalizi ya michuano hiyo baada ya mapumziko ya siku tatu ya maombelezo ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Alisema kikosi cha timu hiyo kinaendelea vizuri na maandalizi ya mchezo huo licha ya kuwapo kwa nyota watatu ambao ni majeruhi wanaotarajiwa kurejea mazoezini wiki ijayo.

"Tunaendelea vizuri na wachezaji wako fiti kwa ajili ya mchezo huo ambao tutakuwa ugenini, kikubwa ni kuhitaji kupata matokeo mazuri ili kufuzu na kucheza fainali ya michuano hiyo," alisema Pawassa.

Alisema kila kitu kinaenda vizuri kwa wachezaji hao kukaa kambini na wako fiti kwa ajili ya mchezo huo wa Machi 30 kabla ya kurudiana nchni Aprili 3, mwaka huu.

Katika mchezo huo, Burundi watakuwa wenyeji lakini utapigwa katika fukwe za Coco jijini Dar es Salaam, baada ya kuomba uchezwe hapa nchini.

# Kiduku ajipa nafasi kumchapa Mkongomani

**Na Shufaa Lyimo**

KUAHIRISHWA kwa pambano la ngumi kati ya bondia Mtanzania Twaha Kiduku dhidi ya Tshibangu Kayembe kutoka DR Congo, lililokuwa lifanyike Machi 19, mwaka huu jijini Dar es Salaam, kumetoa fursa ya kujiandaa vizuri zaidi, imeelezwa.

Pambano hilo ambalo limeahirishwa kutokana na msiba mzito wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, sasa limesogezwa mbele mpaka Aprili 13, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, kutoka mkoani Morogoro, Kocha Mkuu wa Kiduku, Pawa Ilanda, alisema wanaendelea na mazoezi huku wakiwa wanaungana na Watanzania katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo.

"Tunaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na pambano hilo ambalo liliahirishwa kutokana na msiba huu, tunaomba mashabiki wetu waendelee kutuamini kuwa tutafanya vizuri katika pambano hilo ambalo linasubiriwa na wadau wengi wa mchezo wa ngumi,"alisema Ilanda.

Kocha huyo alisema pambano hilo litakuwa la raundi 10 katika uzito wa kilo 76 na kwamba bondia wake kwa sasa anafanyia mazoezi kwenye uwanja wa vijana uliopo mkoani humo ili kuhakikisha mwili wake unakuwa sawa kuelekea kwenye pambano hilo.


Naye Twaha kiduku alisema alishajiandaa kipindi kirefu, hivyo anachokisubiri kwa sasa ni muda ufike apande ulingoni kutoa burudani kwa mashabiki wake, huku akiwaomba wajitokeze kwa wingi kushuhudia kiwango atakachokionyesha.

"Ninaendelea na mazoezi japokuwa nilijipanga mapema kabla msiba huu haujatokea, ninaamini ifikapo siku hiyo ya pambano nitafanya vizuri kutokana na mazoezi ninayoendelea kupewa na mwalimu wangu Pawa Ilanda,"alisema Twaha.

# Michezo

Alhamisi Machi 25, 2021

Nipashe

BALE ATANGAZA KURUDI TENA KUKIPIGA MADRID HABARI UK 22




Baadhi ya wachezaji wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, walipokamilisha mazoezi ya mwisho nchini Kenya juzi, kabla ya kutua Malabo, Equatorial Guinea, tayari kwa mechi ya leo dhidi ya wenyeji hao kuwania kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) mwakani nchini Cameroon. **MPIGAPICHA WETU**

# SAMATTA, KOCHA WATOA NENO DIMBANI BILA JPM

## ●●●Kumuenzi wakiivaa Equatorial Guinea leo ugenini, wasema ni vigumu lakini...

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuwa katika majonzi makubwa ya kumpoteza aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na shabiki namba moja wa Taifa Stars, Dk. John Magufuli, kikosi cha timu hiyo ya taifa kimepania kumuenzi kwa ushindi kitakaposhuka dimbani leo ugenini Equatoria Guinea kuwavaa wenyeji hao.

Katika mechi hiyo itakayopigwa leo majira ya saa nne usiku kwa saa za Afrika Mashariki, Taifa Stars kwa mara ya kwanza itashuka dimbani kucheza dhidi ya Equitorial Guinea, ikiwa inaomboleza msiba wa Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu kwenye Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam kutokana na maradhi ya moyo.

Stars itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Estadio de Malabo nchini huko kwenye mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) zitakazofanyika Januari na Februari mwakani nchini Cameroon.

Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen, amesema amekiandaa kikosi chake kwa muda wa wiki mbili na ana imani kitafanya vizuri kwenye mechi hiyo.

"Tutapamba na Equitorial Guinea. Nafikiri tukishinda itakuwa vizuri sana. Wachezaji wako vizuri na wanataka kwenda kwenye fainali za AFCON... tutapambana," alisema Poulsen.

Nahodha wa timu hiyo Mbwana Samatta, alisema wanafahamu umuhimu wa mechi hiyo, hivyo hawatapambana kizembe.

"Nimeshawahi kufanya kazi na Kim. Mfumo wake naufahamu kwa sababu nimeshawahi kufanya naye kazi. Siku zote yuko vizuri, ni kocha mwenye maono.

"Mchezo tunaokwenda kucheza utakuwa mgumu kwa sababu ni kama fainali na hata wenyeji wetu wanalifahamu hilo na wanataka kutumia kila njia, hasa kwa kuwa wako nyumbani kutaka kupata ushindi. Tumejiandaa vizuri na tunafahamu kama mchezo huu ndiyo utakwenda kutupa nafasi ya kushiriki tena kwa mara nyingine tena Fainali za AFCON, hivyo hatutapambana kizembe," alisema Samatta.

Makocha wasaidizi wa Stars kwa upande wao, wameonyesha masikitiko kutokana na kwenda kucheza mechi hiyo bila Magufuli ambaye wakati wa uhai wake akiwa rais, aliwaambia kuwa yeye ni shabiki namba moja wa Taifa Stars.

"Tunakwenda kucheza mechi hii katika mazingira magumu. Tumekuwa kwenye kipindi kigumu kumpoteza kiongozi wetu wakati tukiwa tunamhitaji sana, tutamkumbuka kwa mengi, lakini yote hii ni kazi ya Mungu," alisema Selemani Matola.

Akimzungumzia Rais wa sasa, Samia Suluhu, Matola alisema kuwa ana imani naye kuwa atafuata nyayo za mtangulizi wake, kwani naye alikuwa anajishughulisha pia na michezo tangu awali.

"Kwenye michezo amekuwa ni mlezi wa timu za wanawake, sasa atakuwa anaangalia timu zote za wanawake na wanaume na nina uhakika kama alianzia huko kwenye michezo, ina maana anaifahamu vilivyo na haitamwia vigumu kuwa mlezi wa wote," alisema Matola.

Naye Juma Mgunda alisema: "Kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu kifo tumeumbiwa sisi binadamu. Ameondoka rais wetu kipenzi. Mimi binafsi nitamkumbuka kwa sababu alishatangaza kuwa yeye ni shabiki namba moja wa Taifa Stars. Leo hatunaye. Tena amefariki wakati sisi hatupo nchini, inauma sana."

Kwenye Kundi J, Tanzania inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi nne, wakati Tunisia ambayo leo itakuwa ugenini dhidi ya Libya, ikiwa kileleni na pointi 10. Equitorial Guinea yenyewe ina pointi sita katika nafasi ya pili wakati Libya inaburuza mkia na pointi zake tatu.

# SIMBA KINARA WA MABAO LIGI ZOTE TZ

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, timu ya wanaume ya Simba na ya Wanawake, Simba Queens, wamebamba kila kona kwa upande wa kucheka na nyavu kwenye ligi hizo kuu hapa nchini.

Hadi sasa Simba ambayo inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 46, nne nyuma ya vinara Yanga yenye alama 50 lakini ikiwa mbele michezo mitatu, ndiyo inayoongoza kwa mabao ya kufunga na hata ya kufungwa.

Simba imefunga mabao 46 na kuruhusu nyavu zao kutingishwa mara tisa tu huku Yanga ikifuata kwa mabao 36 ya kufunga na 14 ya kufungwa.

Kwa timu ya wanawake, Simba Queens ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 39, mabao 65 yakufunga na saba ya kufungwa, wakati ligi hiyo ikiwa raundi ya 15, ikifuatiwa na Yanga yenye alama 38, lakini ikizidiwa mabao ya kufunga na JKT Queens yenye pointi 36. Yanga ina mabao ya kufunga 50 na sita ya kufungwa wakati JKT Queens hadi sasa ikiwa imecheka na nyavu mara 52 na kuruhusu nyavu zake kutikiswa mara 16.

Lakini washambuliaji wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao ndio wanaoongoza kwa kucheka na nyavu kwa timu ya wanaume na wanawake kwani kwa Simba, Meddie Kagere na John Bocco wapo kileleni kwenye orodha ya wafungaji kila mmoja akiwa na mabao tisa wakifuatiwa na mastraika wa Azam FC, Prince Dube na Idd Nado kila mmoja akiwa na mabao nane.

Kwa upande timu za wanawake, mshambuliaji wa Simba, Oppah Clement anaongoza kwa ufungaji akiwa na mabao 25, akifuatiwa na Aisha Juma wa Alliance Girls mwenye mabao 21 na Fatuma Mustafa (JKT Queens) mabao 20 huku kwa upande wa Yanga akiwa ni Aisha Masaka aliyecheka na nyavu mara 19.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002